# Building Bridges to a United Kenya/
# Mapatano na Maridhiano ya Kuunganisha Wakenya

## ANNEX 1: Detailed Recommendations

## Kiambatisho cha 1: Mapendekezo kwa Upana

### Maadili ya Kitaifa

| | Suluhisho | Hatua inayohitajika |
|---|---|---|
| 1 | Wakenya wanahitaji kuwaza sana. Uchaguzi utakuja na kutoweka ukiwa na tawala tofauti ila Kenya itabaki. Tunahitaji maono ya Kenya tunayoitaka katika kipindi cha vizazi vitatu vijavyo au kwa miaka mia moja ijayo: nchi inayotoa msaada wa kipekee kwa watu pengine kwa kuwa dalili ya uhai wa ustaarabu mpya wa Afrika kote barani unaotikisa, wenye kufana na wa kuaminika. | Ni sharti tujadiliane kwa upana kwa njia jumuishi ya mazungumzo ya kitaifa kufikia kilele katika mkutano mkuu kwa lengo moja tu la kuunda maono ya ustaaraabu wa kipekee wa Kenya katika karne ijayo. |
| 2 | Wakenya lazima wabadilike na wawe watu wenye heshima kwa wenzao na washiriki huduma zinazoonyesha uadilifu. Kwa mtazamo huu, Kenya kwa sasa ina upungufu wa uongozi katika viwango na sekta kadhaa, zikiwemo serikali, asasi za kiraia, na sekta ya dini. Kama nchi, tunahitaji kuimarisha uongozi katika matawi yote ya serikali kwa kujenga utaratibu unaoondoa yasiyokubalika, kukuza uzoefu unaofaa, mafanikio, na uadilifu na kutoa njia wazi katika uongozi.<br>• Badala ya mchakato wa juu chini, tunafaa kujenga maadili ya nchi kutokana na maadili yaliyopo katika tamaduni za jamii za Kenya ambazo zina michakato wazi ya kuendeleza uongozi, huduma, na uhalali. Hili linafaa kuunganishwa na taifa kutoka chini hadi juu kwa kuheshimu utofauti.<br>• Lengo ni kukuza uongozi nchini kama njia ya huduma na uadilifu kwa wengine. | 1. Familia, ulezi na ushauri: Kunahitaji kuwa na lengo jipya ya kufundisha maadili, pamoja na kweli ambazo umuhimu wake ni kwa jamii.<br>2. Wazee na viongozi wa kitamaduni wanahitaji kuimarisha maadili ya huduma na jamii yanayopitishwa kwa vijana ikiwemo sehemu ya kijamii katika matambiko ya kitamaduni na kijamii ya kuingia utu uzimani, kama vile sherehe za jandoni. Kwa njia hii, mifanyiko ya kitamaduni na ya kijamii, matambiko, na filosofia ya huduma na uadiliffu zitaunganishwa na taifa. Kunahitaji kuwa na nguvu maalum za kutia mwito wa huduma na uadilifu, kama wananchi katika sherehe zote za desturi za hadi utu uzima katika jamii za kitamaduni na kidini Kenya.<br>3. Makundi ya kidini pamoja na makanisa, misikiti na mahekalu yanafaa kuimarisha maadili ya taifa kwa kuyaingiza katika shughuli zao zote. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 4. Vyombo vya habari: Kenya inahitaji vyombo vya habari vinavyotuwezesha kukua kwa kuwekeza katika ubora wa habari maalum. Vyombo hivi vinafaa kutengeneza maonyesho kwa kuzingatia historia ya Kenya ili kutujuvya upekee wetu.<br>5. Shule: Wakenya wanahitaji kujifunza huduma kutoka kwa wahenga/wazee. Katika shule haswa zile za kulala wanafunzi wanafaa wapewe majukumu na kazi zinazohitaji kujitoa kwao na kuhudumu katika jamii.<br>6. Wanafunzi wote wahusike katika ari za kujitolea zinazohudumia wahitaji na maskini nje ya maeneo ya shule. Ari hizi zinahitaji kuangazia maadili ya huruma, kuhisi maono ya wengine, ushirikiano, na kuwajibika.<br>7. Mfumo wa Kitaifa wa Kujitolea unaotambua mahitaji ya wajitoleao uundwe na utoe vyeti kwa kazi iliyofanywa. Teknolojia itumike kutambulisha mahitaji ya wanaojitolea na kuunganisha mashirika na makundi katika mashule, manyumbani na mahali pa kazi.<br>8. Shuleni wanaojitolea na washauri wajihusishe pamoja na wanafunzi. Likizo zinaweza kutumika kwa kufanya kazi za kujitolea katika mazingira tofauti na yale ya shule.<br>9. Ni lazima kuwe na mtalaa wa lazima - katika kipindi chote cha elimu rasmi ya Kenya – unaofundisha mwanafunzi akiwa bado mchanga maadili ya taifa yaliyokita mizizi katika uadilifu. Mwanafunzi asifuzu kabla ya kuendeshwa kwenye kozi hii.<br>10. Maeneo ya kazi nayo yakumbatie ari za wajibu wa kijamii kwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | ushirikiano unaohusisha shughuli za kujenga maadili ya kitaifa. |
| 3 | Kuunda na kutekeleza mbinu za utekelezaji wa sheria ya uongozi na uadilifu inayohusika na uvunjaji. Tumepoteza njia katika utekelezaji wa sura ya 6 kuhusu Maadili ya Kitaifa na mbinu zilizopo ni chache. | 1. Kuimarisha Sheria hii ili kuhakikisha inatekeleza vyema Sura ya sita (6) na ikiwezekana ibadilishwe na sheria nyingine.<br>2. Mbinu za utekelezaji ziwe katika sehemu zote za umma na haswa kwa tume za huduma kama ya Umma, Bunge, Kimahakama, na Kipengee cha 235.<br>3. Tume zote za huduma zitekeleze wajibu wa Sura ya 6 na sheria ya uongozi na uadilifu – hsawa kwenye michakato ya kuadilisha, mikataba, kuwasiliana na walalamishi, kufanya mikataba upya na kupandishwa cheo kwa kuangazia tathmini zisizopendelea za utiifu. |
| 4 | Kuimarisha uwezo wa uonozi wa kitaifa katika kiwango cha baraza la mawaziri kwa kuchagua watu wanaofurahia heshima ya umma na kitaaluma. | 1. Mawaziri wote wawe na rekodi inayoonyesha uadilifu inayowapa heshima kwa umma na kwa maafisa wanaofanya kazi chini yao.<br>2. Maraisi wote watoe Kanuni za Maadili kwa mawaziri zinazofunga mawaziri wanaochanguliwa katika baraza la mawaziri na zinazoangazia maadili na tabia za kitaifa. |
| 5 | Kuunganisha maadili ya kitamaduni na tabia za wakenya zinazoangaziwa katika desturi za kuingia kwenyee utu uzima hadi kwa maadili na misingi ya katiba na haki na wajibu wa uraia. | Wizara ya Utamaduni na Urithi ihimize baraza zote za wazee au viongozi wa jamii nchini kote wafanye rasmi desturi hizi za kitamaduni na kujumuisha jinsia zote na kuwahusisha katika majukumu maadili ya kitaifa na haki za raia. |
| 6 | Kuwe na uwiano kati ya tamaduni zetu tiofauti na utambulisho wa Kenya ya sasa ili kusiwe na tofauti za kindani. | 1. Kuimarisha wizara ya Utamaduni na Urithi. Jamii inayokuza maadili yao ya taifa itahakikisha jambo hili ni muhimu sana katika vijenzi vya serikali. Sikukuu ya "Boxing day" ya tarehe 26 Disemba ibadilishwe na kuwa na siku ya kitaifa ya utamaduni ili kusherehekea tamaduni zetu na kujifahamisha tamaduni za wakenya. (pengine pia kwenye tarehe moja Januari) |

| | | |
|---|---|---|
| | | 2. Wazee waunganishwe kwa pamoja na pia kwenye mashirika ya umma kupitia kwa kongamano zitakazojadili jinsi utamaduni utasaidia ari za sera na uhusiano wa kimkoa.<br>3. Baraza za wazee za kitaifa ziwezeshwe kushiriki pamoja na wenzao katika mahusiano ya kimkoa, bara na kimataifa kuhusu masuala kama vile uongozi wa kimaadili; ulezi unaowajibika; matumizi ya desturi za kuingia kwenye utu uzima ili kuimarisha uraia; mazungumzo na heshima kati ya jamii tofauti; kuzuia migogoro, kupatanisha, na suluhisho; kulinda urithi na historia; maadili na uadilifu. Haya yafanyike kupitia kwa unganisho zinazotolewa na wizara ya masuala ya nje, wizara ya utalii, bodi ya haki ya kunakili, huduma ya wanyamapori, na sehemu nyinginezo mahususi za serikali.<br>4. Kuunganisha wazee na mifumo rasmi ya kupanisha inayokubalika na mfumo wa kisheria kwa kuwafundisha na kuwapa vyeti na pia kuwaungisha na taasisi za kimahakama na serikali kote nchini.<br>5. Wizara ya utamaduni na urithi itumie ushiriki wa umma na pembejeo maalum ili kuweka mpangilio rasmi wa miungu yote ya mashujaa wa Kenya wanaoonyesha maadili ya Kenya, vita vya uhuru na demokrasia, matarajio yetu, na ushindi wetu unaoonekana. Mashujaa hawa wawekwe kwenye chumba cha makumbusho, kwenye mitaalaa na kwenye maonyesho.<br>6. Mashujaa wanaotambulika rasmi walio hai wapewe msaada iwapo hawajiwezi. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 7. Kila kaunti iwe na Sheria ya Utekelezaji wa Kuhifadhi Maarifa ya Kimapokeo na Hisia za Kitamaduni ya 2016 kwa kutoa shughuli za kitamaduni na vituo vya kusherehekea utamaduni katika kaunti na pia katika kiwango cha kitaifa. |
| 7 | • Ni wajibu wetu kujenga ustaarabu wa nchi unaotetemesha kwa kujitengenezea karama ya kujuwa, kuheshimu, na kujihusisha na historia zetu tofauti.<br>• Sehemu kubwa ya unyonge wa Afrika na uvunjaji moyo huibuka kutokana na historia zetu kuelezwa na makundi ya watu ambao wametutawala na kuamua kusaidika kutokana na sisi kuwa wapuuzaji, kugawanyika na kutojihamasisha.<br>• Kama ijulikanavyo kote ulimwenguni, watu wasiojua wala wasioweza kueleza hadithi yao hawawezi kufahamu ukubwa wao. Hivyo basi tunapendekeza kuwa wakenya wajipe historia yao rasmi iliyo bora kabisa. | 1. Makavazi ya Kitaifa ya Kenya na huduma ya hifathi ya hati ibadilishwe jina na kuitwa Huduma Rasmi ya Makavazi ya Kihistoria na Kitaifa.<br>2. Makavazi haya mpya yawe na jukumu pana na kuwa sehemu ya kati ya jitihada za kushirikiana na za kitaaluma kutoka kwa maktaba, vyuo vikuu, vyumba vya maonyesho, na wanahistoria binafsi kufanya utafiti, kuchunguza, na kuwasilisha historia ya Kenya iliyo bora kabisa kwa Wakenya na ulimwengu mzima.<br>3. Taasisi hii iongozwe na msomi wa historia ya Kiafrika mwenye hadhi ya juu au mtaalamu hodari anayefahamika ulimwenguni kuhusu masuala ya sayansi ya maktaba. Iwe na bodi yenye kuwakilisha wizara ya Urithi na ile ya Elimu; vyuo vikuu vya nchini na vya kigeni; vyumba vya makumbusho vya kihistoria na urithi nchini na vya kigeni; waangalizi wa jumba la makumbusho; wasanii; na wazee.<br>4. Rais Uhuru Kenyatta anafaa kufungua historia rasmi ya Kenya ambayo matokeo yake yataongozwa na afisi na mkaaji wa Historia katika makavazi ya Kitaifa. Historia hii inafaa kuangazia miaka 1000 iliyopita na kutoa maelezo sahihi na yenye fasili ya ulowezi wa wakaaji wa sasa wa Kenya; urithi wa kisiasa, |

| | | |
|---|---|---|
| | | kiuchumi, na kitamaduni wa makundi yote kiukoo nchini; dhima ya mwanamke katika historia; maelezo ya ukoloni na biashara za utumwa za kimataifa; mapambano dhidi ya ukoloni; historia ya baada ya kupata uhuru ya kila sehemu ya nchi; na historia za kisasa pamoja na zile za mijini na jamii mpya zilizoundwa nchini Kenya.<br>5. Katika Makavazi haya, kuwe na maafisa wafanyikazi ambao ni wataalamu wa kihistoria, wakutubi, waangalizi wa jumba la sanaa, na wataalamu kutoka kwenye Nyanja za kistadi zenye mahusiano kama vile, filosofia, lugha, anthropolojia, elimu ya dini, wanahistoria wa kiuchumi, siasa na sayansi.<br>6. Kazi iunganishwe na malengo ya vyumba vya makumbusho vya kitaifa, vituo vya kitamaduni vyenye kupata misaada ya umma, wizara ya elimu, baraza zote zinazojihusisha na ukuzaji wa mtalaa, mafunzo, na elimu ya wakenya.<br>7. Kazi yake iundwe ili iweze kueleweka na wakenya wote haswa wanafunzi na wanarika.<br>8. Shirikiana na kuungana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni katika kujenga juhudi hizo. |
| 8 | Sharti kazi iakisi au idokeze tabia na ujuzi na iwe njia ya kujiheshimu na hadhi ya binafsi hata tunapojitahidi kuongeza nafasi za kazi na viwango vya kiuchumi. | 1. Elimu ya kiufundi na TVET inahitaji kuundwa upya ili ifundishe thamani ya ufundistadi kama kuwa bora kuliko ajira na mapato – huakisi ustadi na tabia.<br>2. Kutoa mwongozo wa utambuzi wa ufundistadi na mpangilio wa ustadi ulio wazi, wenye usawa na unaoweza kupatikana kwa urahisi.<br>3. Kuramani kaunti zote ilim kuwa na ustadi wa kipekee wa ufundi; |

| | | |
|---|---|---|
| | | kuikuza, kuboresha ujuzi wake, na kuiunganisha na masoko.<br>4. Kuramani viwanda vya kipekee katika kila kaunti na kupanua nafasi kwa kuhimiza mwingiliano mzuri kwenye masoko, kuimarisha ujuzi wa vijana, na kuingiliana na viwango vya juu. |
| 9 | Furaha, uzima, na afya ya kiakili ya wakenya inafaa kupewa msaada unaofaa. | 1. Wizara ya Afya inafaa kuwa na idara ya furaha, uzima, na afya ya akili inayotolewa ili kushughulikia sera na viwango wa maeneo haya. Zikuzwe kwenye kaunti zenye majukumu ya afya. Iunganishwe pia na wizara ya utamaduni ili kuhakikisha kuwa program na mitazamo imefahamishwa na taasisi za kitamaduni za Kenya na mtazamo wa uzima na afya ya akili.<br>2. Kama sehemu ya kazi ya Kiwango cha Maendeleo ya Watu, Kenya inafaa kuwasilisha kiwango kilichoachana cha furaha. |

**Haki na Majukumu**

| | Suluhisho | Hatua inayohitajika |
|---|---|---|
| 1 | Wakenya wana haki walizopewa na Mungu ambazo zinahitaji kuambatana na Mkataba wa Kenya wa Majukumu. | 1. Kwa kuongozwa na wimbo wa taifa na maadili ya kitaifa, mkataba wa majukumu ya raia uundwe ukujumuisha ahadi za kiuzalendo kwa taifa na katiba ya Kenya (kwa shule, kazini katika sherehe rasmi na mikutano ya wananchi)<br><br>2. Mkataba usiwe wa maneno tu bali ueleze kwa ufasaha ni nani mkenya halisi na anavyohusiana na wengine. |
| 2 | Malezi yaliyoelimika ni muhimu katika kukuza watoto walio na afya na waliojukumika katika Kenya inayokua kwa kasi na yenye utata kueleweka. | 1. Kanisa nyingi zinasisitiza kuwa wana-ndoa wahudhurie mafunzo kabla ya kufunga ndoa, kuhakikisha wamejua jinsi ya kulinda ndoa; |

| | | |
|---|---|---|
| | | juhudi hizi ni muhimu katika kuimarisha malezi.<br><br>2. Kikosi maalum cha mawaziri kinafaa kiundwe ili kibuni mtalaa wa malezi na pia kuifanya iwe inapatikana katika majumba ya kidini na utamaduni, vituo vya afya, kwa naibu wa chifu, na kwa chifu ili iweze kuwafikia watu wengi kwa muda ufaaao. |
| 3 | Mojawapo ya kuchaguliwa kuwa Waziri au Katibu Mkuu, na wasawa wao katika majimbo, ni kuwa tayari kuwa na “ngozi ngumu” kwa kutumia huduma wanazobuni na kuziungama kwa niaba ya wakenya wote. Kama ni njema kwa wakenya, zapaswa kuwa nzuri kikamilifu kwako. | 1. Kanuni ya kiuwaziri yafaa iwahusishe mawaziri wanaohusika na kuzitumia huduma hizo ili kujifaidi. Kwa mfano, watoto wa waziri wa elimu wanafaa kuhudhuria na kusomea shule za umma. Waziri wa afya anapasa kutumia hospitali za umma, na kadhalika. Mawaziri wote wanafaa kutumia huduma na vifaa vya umma.<br><br>2. Hizi kanuni zapaswa kuashiriwa katika majimbo na mawaziri wa kaunti. |
| 5 | Sehemu kuu ya majukumu ni kwa watoto. Kukiukwa haki au kuteswa na wazazi, au yeyote mwenye umri mkubwa, yafaa kuadhibiwa vikali kisheria na kutiwa aibu kwa wanakijiji. Aidha, ni jukumu la kitaifa kuhakikisha hakuna mtoto ametelekezwa au asiye na makao. | 1. Adhabu ya kumtelekeza mtoto yafaa kutekelezwa na kua kali mno.<br><br>2. Tia nguvu mbinu za kuwalinda watoto na kuwasaidia waliotelekezwa. |
| 6 | Kuna haja ya dharura kuendeleza na kutandaza elimu ya kiraia kuhusu haki na majukumu. | 1. Elimu kwa raia yafaa kupewa kipao mbele kwenye sera za serikali na uvumbuzi wake, kitaifa na pia katika majimbo. Hii inajumuisha kampeni dhahiri zinazoendelea na iko na msingi kwa mbinu zinazoweza kufikika ambazo hazihitaji muundo-msingi kufikika, kwa mfano; kupitia kwa baraza.<br><br>2. Elimu kwa wananchi yafaa kutolewa katika viwango vyote vya elimu. |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | Kusisitiza uelewa wa maadili, mafunzo, na uwajibikaji katika maeneo ya kazi | Kila taasisi ya umma, shirika lisilo la serikali na kampuni yafaa kubuni uadilifu na mikakati ya maadili ambayo inahusu mafunzo, na njia salama za kuripoti uvunjaji sheria na pia ihusishwe katika upimaji wa vitengo na wasimamizi wake. |
| 8. | Kuwa na tabia ya uwajibikaji na utekelezaji kwa wakenya wote wa umri mdogo. (Kuna upungufu kitaifa katika utekelezaji na kukubali uwajibikaji. Desturi ya kuwajibika na utekelezaji kikamilifu wake sio yenye umaizi: Inafaa kukuzwa katika watu kutoka wanapolelewa na kukua, maadili na utangamano wetu wa kitaifa, na katika mafundisho na elimu) | 1. Shule za Kenya zafaa kuwaleta wanafunzi wote katika kazi ndogo ndogo za kila siku na majukumu yanayoinua shule na jamii kwa jumla. Hii itasaidia kupalilia desturi ya uwajibikaji.<br>2. Vitengo vyote vya shule, vyafaa kuwarai na kuwawezesha wanafunzi wanaojitolea kwa wenye mahitaji katika jamii ama taasisi zilizoko karibu na shule. |
| 9. | Wakenya wote wanafaa kutenga miezi sita ya maisha yao kwa huduma ya taifa kati ya umri wa miaka 18 na 26. | 1.Vitengo vya serikali vyafaa kubuni jukumu la kijamii la pamoja linalohusiana na jambo hili.<br>2.  Tia moyo vikundi vya kujitolea katika shule zote.<br>3. Mikakati yafaa kubuniwa ya kuwahusisha wale ambao hawako shuleni.<br>4. Kunafaa kuwa na mtandao wa kitaifa wa kujitolea unaokubali juhudi zinazohitaji wakujitolea watie saini na kuwaelekeza kwa wale wanaotaka kuifanya kazi. Mtandao huu unafaa kuwapa vyeti baada ya kumaliza muda wa kujitolea kwao. Motisha, kwa kupitia kuifanya kama matakwa ya kuomba kazi ya utumishi wa umma, yafaa kuzingatiwa. |
| 10. | Haki na Majukumu ya wananchi yafaa kujumuishwa katika hatua za kutia mtu jandoni kitamaduni, kidini, na kijamii na katika elimu ya kitamaduni na ya kidini. | Wizara ya Utamaduni na Urithi yafaa kuhakikisha kila sherehe za kidesturi/kitamaduni zina sehemu ya haki na majukumu ya Mkenya. |
| 11. | Uzima wa akili ni muhimu sana kwa taifa lenye afya yenye raia wanaohusika. | Kamati maalum yafaa kubuniwa kutafuta suluhu ya kufanya matibabu ya akili kufikika, kupunguza aibu kwa wanaoumia, na msaada kwa wanaopeana huduma za kinyumbani. |

**UHASAMA NA USHINDANI WA KIKABILA**

| | Suluhisho | Hatua inayohitajika |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| **1** | Ondoa modeli ya mshindi-kuchukua-yote katika utendaji wa kitaifa | Hakikisha utendaji wa serikali unaangazia mwonekano wa Kenya na unatekeleza kwa pamoja utashi wa kisiasa wa wakenya badala ya kufanya uteuzi kwa misingi ya ukabila. |
| **2** | Kuunga mkono jukumu la raisi kama ishara ya umoja wa kitaifa | Kuunda baraza la washauri lenye watu wenye utumishi bora na unaoheshimika katika huduma ya umma, sekta binafsi, akademia, sanaa na michezo, sekta ya dini, na wazee walioheshimika. Itatoa ushauri wa faraghani kwa Mkuu wa Taifa kuhusu jinsi ya kudumisha umoja wa taifa bila malipo yoyote. |
| **3** | Kuhakikisha makundi ya kisiasa yamejumuishwa kikabila kuhusu uwanachama na mbinu za kuingia kwenye uongozi na yaongozwe ili kuhakikisha hayatatumika kama chombo cha utengano wa kikabila. | Kuunda mbinu za utekelezaji katika Sheria ya Makundi ya Kisiasa. |
| **4** | Kushughulikia kwa haraka migogoro inayoweza kujitokeza kuhusu malisho na maji zinazotenganisha jamii na kupanua uhasama wa kikabila. | 1. Kamati ya kitaifa ya kujenga amani kuanzisha na kutekeleza taratibu za kukabiliana na kutaarifu mapema kuhusu migogoro inayohusiana na mali katika mfumo wa kitaifa wa kukabiliana na dharura, majanga na mgogoro.<br>2. Kuimarisha taratibu za kukabiliana na kutaarifu mapema za mipakani na kuratibu jinsi wizara kadhaa hupanga na kutekeleza program zao katika maeneo yenye ukame na yenye ukame kiasi.<br>3. Kuimarisha uhusiano wa taratibu za kukabiliana na kutaarifu mapema na wazee na kamati za amani ili kupunguza muda upoteao kabla ya kuchukua hatua ya kuzuia mgogoro. Vile vile kukubalia wanachama wa kamati ya Amani kuwasilisha habari za siri zilizolindwa. |
| **5** | Kuzidisha heshima kwa utofauti wa kabila na dini na kushikilia vyama vingi. | 1. Mitalaa kote katika mfumo wa elimu iangazie vipengele vya lazima kuhusu historia; tofauti za tamaduni; ujuzi wa dini kuu pamoja |

| | | |
|---|---|---|
| | | na za kiasili; na uhusiano kati ya katiba na tamaduni/dini zetu.<br>2. Hakikisha kwamba shule za sekondari za kulala ambazo zinafadhiliwa na umma zinao uwakilishi wa kaunti zote na kuunda asilimia hamsini (50%) ya wanafunzi.<br>3. Oanisha misheni hii na majumba ya kitaifa ya makumbusho.<br>4. Kukuza na kusaidia vituo vya utamaduni vya pamoja katika kila kaunti. |
| **6.** | Kuzidisha mtagusano na ufahamu wa tofauti za wakenya haswa baina ya wanafunzi ili kuturuhusu kuwa na ushirikiano zaidi. | Wizara ya elimu inafaa kuhakikisha kwamba mashule ya kulala na vyuo vikuu vina wanafunzi kutoka pande zote za nchi. Kunafaa kuwa na juhudi maalum za kuunganisha mashule ili kujumuisha jamii zinazojulikana kung’ang’ania rasilmali adimu kama maji na malisho. |
| **7** | Kutumia vizuri taratibu mbadala za kutatua migogoro inayopunguza migogoro na mgawanyiko. | 1. Kutoa mafunzo kwa wazee na usajili rasmi kama wapatanishi wanaofahamika na mfumo wa sheria.<br>2. Kuhamasisha mahakama kuwa na vijumba kwenye mahakama kote nchini vitumiwe na wapatanishi walioteuliwa kutoka kwa wazee. |
| **8** | Kubadilisha kalkulasi yetu ya siasa za kikabila kwa kuendesha mfumo wa kuunganisha jumuiya ya Afrika Mashariki. | Kama njia za kuunganisha tena jamii za mipakani na kubadili kalkulasi yetu ya sasa ya siasa za kikabila huku tukijenga uchumi bora zaidi, kuharakisha mchakato wa shirikisho la jumuiya ya Afrika Mashariki kama hatua ya shirikisho la siasa. |
| **9** | Kuhamisha misheni ili kuimarisha ushirikiano na upana wa kitamaduni katika baraza la mawaziri ili kuliwezesha kuwa na jukwaa kubwa la utekelezaji. | Kuhamisha majukumu ya Kituo cha Habari cha Uhalifu cha Kitaifa ya ushirikiano hadi kwa Wizara ya  Utamaduni/Urithi, Wizara ya Elimu na MDA na tume zinazokabidhiwa elimu ya uraia. |
| **10** | Kuhakikisha sura ya Kenya inashuhudiwa kwenye ajira ya sekta ya umma katika vyeo na idadi, kulingana na katiba. | Pasipo na mgombea mwenye sifa zinazohitajika, Tume ya Huduma ya Umma inafaa kuwezeshwa kutafuta wagombea wengine wenye ustadi ili kuongezea fursa ya kuhitimu kwenye nafasi hizo. |

| | | |
|---|---|---|
| **11** | Kusaidia afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa kuwa yenye haki, huru na yenye kujitegemea. | Kuimarisha Msajili wa Vyama vya Kisiasa kwa;<br>1. Kukomesha uteuzi wa watu kwa niaba ya msajili.<br>2. Kuajiri msajili wa kudumu.<br>3. Kuimarisha uwezo wa afisi ya msajili wa kufuatilia na kuadhibu wanasiasa na vyama vya kisiasa vyenye kueneza chuki na kuchochea ukabila.<br>4. Kuondoa nguvu za kisheria za utekelezaji wa matamshi ya chuki kutoka kwa Kituo cha Habari cha Uhalifu cha Kitaifa (NCIC) hadi kwa msajili wa vyama vya kisiasa na Kurugenzi ya Uchunguzi wa Makosa ya Jinai (DCI) ufikiapo wakati wa kuingilia uhalifu. |

**UCHAGUZI WENYE MIGAWANYIKO**

| | **Suluhisho** | **Hatua inayohitajika** |
|---|---|---|
| 1 | Kufanya muundo wa utendaji kuwa jumuishi zaidi. | 1. Kugombea na kuchukua ushindi wa urais – Rais atachaguliwa kwa kupitia kwa njia ya haki ya kimataifa ya upigaji kura. Ili mgombea wa urais kutangazwa mshindi ni sharti apate ushindi kwa asilimia 50+1 wa kura za rais na angalau asilimia 25 kwa kura za zaidi ya nusu ya kaunti zote, kama ilivyo kwa sasa.<br>2. Rais mtendaji – Rais atabaki kuwa Mkuu wa Nchi na Serikali na Mkuu wa Majeshi. Yeye ndiye atakayekuwa ishara kuu ya Umoja wa Kitaifa. Rais ndiye atakayekuwa mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri, inayoafikiana na Naibu wa Rais, Waziri Mkuu, naa mawaziri.<br>3. Watendaji chini ya uongozi wa Rais watakuwa na uwezo wa kuamua sera ya serikali kwa jumla, nao mawaziri chini ya uongozi wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | Waziri Mkuu watakuwa na majukumu ya Bunge ya Kitaifa ya utekelezaji wa masuala ya serikali.<br>4. Upeo wa Muhula – Kudumisha upeo wa mihula miwili iliyopo kwa nafasi ya Rais.<br>5. Naibu wa Rais – Naibu wa Rais ndiye mgombea mwenza wa Rais. Yeye ndiye atakayekuwa naibu wa Rais. |
| 2 | Rais atateuwa Waziri Mkuu | 1. Siku mahususi kufuatia kuitwa kwa Bunge baada ya kupiga kura Rais atamteua mbunge kutoka kwa chama chenye wabunge wengi kuwa Waziri Mkuu. Iwapo hakuna chama kilicho na wabunge wengi, basi atamteua mbunge atakayeonekana kuungwa mkono na wabunge wengi.<br>2. Idhini ya Bunge – anayeteuliwa kuwa Waziri Mkuu hataweza kuanza kazi kabla ya uteuzi wake kupitishwa katika kikao cha Bunge huku ukiungwa mkono na kura za wabunge walio wengi.<br>3. Iwapo mteuliwa huyo hatapitishwa, itamchukua Rais siku zingine kumteuwa mtu mwingine. Hatua hii itaendelea hadi pale uteuzi wa Waziri Mkuu utafanikishwa. Hatua za kuhakikisha mchakato huu ni dhahiri na utawala ni endelevu zizingatiwe.<br>4. Kuondoa – Waziri Mkuu anaweza kuondolewa ofisini na Rais au kupigiwa kura ya kutotumainiwa kwenye Bunge na kuchukua ushindi wa wengi. |
| 3 | Majukumu ya Waziri Mkuu | 1. Waziri Mkuu atakuwa na mamlaka juu ya udhibiti, usimamizi na utekelezaji wa kazi na shughuli za siku kwa siku za serikali.<br>2. Waziri Mkuu atakuwa ndiye kiongozi wa Biashara za Serikali kwenye Bunge. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 3. Kwa ruhusa ya Rais, Waziri Mkuu atakuwa mwenyekiti wa kamati ndogo za Baraza la Mawaziri.<br>4. Waziri Mkuu atafanya kazi, au kuamuru kazi yoyote ifanywe kwa agizo la Rais.<br>5. Waziri Mkuu atapokea mshahara wake kama mbunge na wala hataongezewa mshahara kwa kuwa na jukumu la Uwaziri Mkuu.<br>6. Katibu mkuu katika ofisi ya Waziri Mkuu atakuwa mwenyekiti wa Kamati ya Utekelezaji wa Kiufundi ya makatibu wakuu.<br>7. Ili Huduma ya Umma kuepuka mwako wa kisiasa, makatibu wakuu hawatahitaji idhini ya Bunge bali wajibu wao utakuwa kwenye ufundi na utawala. |
| 5 | Baraza la Mawaziri iliyochanganyikana | 1. Baraza la Mawaziri ni sehemu kuu sana ya Utendaji wa Serikali. Kutokana na maoni ya Wakenya, mfumo uliopo sasa una upungufu na kikosi maalumu cha kazi kilichopokea maoni haya kilipendekeza baraza ichukue muundo mpya kama ifuatavyo;<br>2. Rais atateua mawaziri baada ya kujadiliana na Waziri mkuu. Mawaziri hawa watawajibika kwenye afisi zitakazowekwa na Rais kulingana na katiba.<br>3. Mawaziri watateuliwa kutoka kwa wabunge na wanateknokrasia pale ambapo wabunge wataondolewa cheo chao kama wabunge baada ya kupata wadhifa mpya.<br>4. Jopokazi inapendekeza pia katibu wa baraza la mawaziri aitwe waziri.<br>5. Ili kuhakikisha mwelekeo wa siasa umekuwa bora zaidi, na kuwa na uwajibikaji wa bunge, kutakuwa na Waziri wa Nchi atakayeteuliwa kutoka kwa wabunge na kutekeleza jukumu lao kama watakavyoagizwa na mawaziri. Mawaziri hawa wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | Nchi wataendelea kupokea mshahara wao kama wabunge bila nyogeza ya mshahara wa wadhifa mpya.<br>6. Cheo cha Katibu Mkuu wa Utawala kiondolewe. |
| 6 | Kuinua hadhi ya upinzani na kuiwezesha upinzani ili kuongeza uwajibikaji wa serikali. | 1. Kiongozi rasmi wa upinzani – mshindi wa pili katika uchaguzi wa Rais atakuwa na wadhifa wa ubunge na kiongozi rasmi wa upinzani iwapo chama chake hakitakuwa kimewakilishwa katika serikali au muungano wa vyama vya bunge ambavyo havijawakilishwa serikalini.<br>2. Haja ya upinzani wenye nguvu – chama au muungano wa vyama visivyokuwa serikalini utakuwa ndio upinzani rasmi.<br>3. Baraza la Mawaziri la Kivuli – kiongozi wa upinzani rasmi ataweza kuwa na baraza lake la mawaziri la kivuli ili kupinga nafasi ya serikali kwenye bunge. Itaweza pia kuwa na nafasi nzuri ya kuchunguza vyema sera na ajenda ya kisheria ya serikali.<br>4. Chama cha upinzani kitakuwa na jukumu kuu la uwaziri mkuu na kuuliza mawaziri maswali kwenye vikao vya bunge. Wakati huu utakuwa ni nafasi ya wabunge kuuliza mawaziri wa serikali maswali kuhusu masuala wanayohusika nayo. |
| 7 | Kufanya mageuzi kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) | 1. Mbinu iundwe itakayowapa viongozi wa vyama vya bunge jukumu katika kutafuta wanatume wa IEBC. Katika kuchagua wagombeaji wa tume, viongozi hawa wachague watu wasioegemea upande wowote wa kisiasa wenye rekodi ya uadilifu na wasiounga mkono wanaharakati wa chama.<br>2. Maoni ya wakenya yaliyofikia jopokazi yanadhihirisha kuwa imani |

| | | |
|---|---|---|
| | | yao kwa tume hii ya uchaguzi na mipaka imefifia. Hivyo basi, jopokazi hii inapendekeza kuwa tujiandae kwa mwanzo mpya kwenye uchaguzi ujao ili kufufua na kuimarisha imani kwenye taasisi hiyo.<br>3. Wanafanyikazi wote wa tume ya IEBC waajiriwe kwa misingi ya mkataba wa miaka mitatu ambayo inaweza kufanywa upya tena mara nyingine moja iwapo utendakazi wao unaridhisha, na usiporidhisha, mkataba uishe kabisa. Jambo hili litasaidia kupunguza makosa kwa kuwezesha kila tume kuajiri wafanyakazi mara moja katika kipindi chao cha kuwa ofisini.<br>4. Maofisaa wote wa kusimamia uchaguzi waajiriwe kama walivyoajiriwa wanakamati kwa njia ya ushiriki umma. Baada ya kuajiriwa kwa maofisaa hao tume hii ipokee ripoti za maamuzi na misingi ya maamuzi hayo na yawekwe kwenye umma.<br>5. Maofisaa hawa watie sahini mkataba wa muda mfupi na wasisimamie zaidi ya uchaguzi mmoja.<br>6. Mtu yeyote aliye na tajriba ya angalau miaka 15 katika viwango vya juu anastahili kuomba kazi ya uanachama wa tume hii. Nafasi hii isihifadhiwe wanasheria tu bali mwanatume mmoja awe mwanasheria.<br>7. Wafanyikazi wote wa tume hii waliopo na wenye vyeo vikubwa wa wapekuliwe.<br>8. Kuainisha majukumu ya katibu na afisa mkuu mtendaji; mwenyekiti wa tume awe ndiye Afisa Mkuu Mtendaji.<br>9. Uundaji wa tume hii udhihirishe picha ya nchi katika kila kiwango. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 10. Kuchunguza njia za kutunga vifungu ambavyo vinapunguza gharama kubwa za uchaguzi wetu. Mfumo wa orodha ya chama ni mmoja wao.<br>11. Kubadili mfumo uliopo wa kupiga kura ilim kuhakikisha umekuwa rahisi, sahihi, hakika, salama, wenye kuwajibika na wazi kama inavyopewa mamlaka na kipengee cha 86 cha katiba. |
| 8 | Uwakilishaji – kusawazisha uwakilishaji na usawa wa uraia kwa kuhakikisha kuwa kila kura ya mkenya ina hadhi na uwezo sawa na kwamba hakuna anayeweza kukana kanuni ya 'kura moja kwa mtu mmoja'. | 1. Chaguo la watu kama inavyoangaziwa katika uchaguzi wa wawakilishi wao, zikiwemo pia katika misingi na uteuzi wa vyama utafanyika kupitia kwa uchaguzi wazi, na wa haki.<br>2. Watu walioko kwenye orodha ya chama watakuwa wamepitia kwenye mchakato unaotumia ushiriki wa umma ulio wazi kwenye kaunti zote hata kabla ya hata upekuzi wowote kufanyika.<br>3. Kutakuwa na usawa kwenye uwakilishaji na usawa wa uraia inavyowezekana kwa kuhakikisha kuwa kila kura ina hadhi na nguvu sawa kulingana na katiba.<br>4. Vyama vitashurutishwa kupititia kwa Sheria yaVyama vya Kisiasa ili vipatane na katiba na kufikia sheria ya jinsia na vipimo vingine vya kikatiba vya ujuishaji kwenye orodha zao za vyama. Hili litasawazisha jinsia zote mbili kisiasa badala ya kuunda mfumo sambamba inayoleta roho ya kianzio.<br>5. Uorodheshaji wa wabunge wa kaunti pia utafuata kanuni hizo na hatua za ushiriki umma, upigaji kura na upekuzi kama bunge la kitaifa. Jambo hili litahakikisha kuna uwajibikaji wa moja kwa moja. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 6. Maeneo bunge yote yakiwa 290 yatanusurika pamoja na viti vilivyolindwa kwa kuwa yamekuwa sehemu kuu ya uwakilishi wa maeneo yenye watu wachache.<br>7. Bomoa vyama vya kisiasa ili kupata matawi ya vyama kwenye kaunti ambapo kutakuwa na nafasi ya wananchi kuendeleza vikao vya kisiasa na vile vile kuhakikisha viongozi waliochaguliwa wamewajibika kila wakati na wala sio wakati wa kupiga kura pekee.<br>8. Uteuzi kupitia kwa vyama ufanyike hadi mwisho kwa uwazi ikitawaliwa na vyama vya kisiasa vilivyo chini ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa na Tume ya IEBC. |
| 9 | Kenya ina upungufu wa uongozi. Pengo hili linaweza kufungwa kwa kuboresha uadilifu katika uongozi na uaminifu kwa wagombea ofisi na wateuliwa wenye vyeo vikubwa ofisini. | 1. Kufichua kwa ukali fedha za umma.<br>2. Wenye hatia na mashtaka ya jinai wasipewe majukumu kwenye uongozi aidha kwa kuchaguliwa au kuteuliwa.<br>3. Mbinu za kutekeleza maadili na kanuni ya katiba yanayotoa kizuizi kwenye tabia. |

**Ujumuishi**

| | **Suluhisho** | **Hatua inayohitajika** |
|---|---|---|
| 1 | Huduma zote za umma ziwakilishe sura ya Kenya kwa kujumuisha mikoa, makundi ya kikabila na dini tofauti. | 1. Ajira serikalini (matawi na viwango yote) iwe kwa wanaostahili na iangazie makundi ya makabila nchini.<br>2. Pasipokuwepo na mgombea aliye na sifa zinazohitajika, Tume ya Huduma ya Umma na Kipengee cha 235 cha Serikali za Kaunti zinahitaji kuwezeshwa ili kufanya uchunguzi wa kitaaluma na kukuza |

| | | |
|---|---|---|
| | | wagombea wachache ili kuongezea uwezo wao wa kufaa kwenye nafasi hizo.<br>3. Kwa kuzingatia huduma na vikosi vya nidhamu, muungano wa kampuni za kibinafsi za kuajiri zenye sifa nzuri kimataifa zizingatiwe ili kusaidia kujaza pengo la uajiri katika huduma za kinidhamu kwa kuzingatia sura ya nchi.<br>4. Tume ya Huduma ya Umma iwezeshwe kuweka kwa umma ripoti yake ya kila mwaka kuhusu utofauti katika Huduma ya Umma. |
| 2 | Nguvu sawa za kura, au “mtu moja,kura moja” ndio kigezo halisi cha demokrasia ya uchaguzi. | Ili kuwepo kwa usawa wa uwakilishi, ambayo ni kigezo muhimu cha ujumuikaji, kila kura ya mkenya inafaa kwa vyovyote vile kuwa na nguvu sawa katika sanduku la upigaji kura. |
| 3 | Tumia orodha ya chama na uwakilishaji sawa ili kuhakikisha sheria ya jinsia kwa uongozi wa serikali ya kitaifa na kaunti, waliochaguliwa na kuteuliwa na kuhakikisha uwakilishaji wazi wa wanawake katika nyadhifa za uongozi. | 1. Mgombea kiti cha ugavana akiwa ni mwanaume, mgombea mwenza awe ni wa kike, na kinyume chake.<br>2. Angalia mapendekezo mengine chini ya “Uchaguzi uliogawanyika” |
| 4. | Imarisha mfumo wa kisheria ili kusaidia kushurutisha na kuweka kikwazo kwa kutowajibika kwa maadili ya kikatiba na kanuni za utendaji kazi wa umma. | Mapitio ya kisheria ili kuipa nguvu PSC na vitengo vingine vya utekelezaji, mahali pa malalamishi kwa umma, na urekebishaji wa tabia kwa wasiotii kanuni na maadili ya kitaifa. |
| 5 | Tamaduni na uridhi wa jamii za kenya zinafaa kuheshimika na kukuzwa na nchi. | 1. Wekeza katika kukuza na kujenga uaminifu katika hekima ya kindani, ujuzi wa kitamaduni uliozingatiwa katika mila na mienendo, vyakula na dawa.<br>2.Wizara ya Utamaduni na Urithi yafaa iwezeshe utafiti, urembeshaji vinyago, na kuonyesha utamaduni kadha wa kadha wa Kenya kwa njia ambayo itaelekea kuelewa kwa hali ya juu na kuuheshimu.<br>3. Jumba la kitaifa la ukumbusho la Kenya yafaa kufanya jarida nene na kuonyesha urithi wa nchi hii na pia utamaduni unaoibuka ambao ni mseto wa mila na mbinu za kuishi. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 4. Majimbo yanafaa kuhimizwa kuwa na jumba ka kumbukumbu la mila na siku za mila ambazo zitajumuisha tofauti za watu.<br>5. Hekalu rasmi ya miungu yote ya mashujaa yafaa kutumiwa katika taasisi za elimu na elimu ya umma.<br>6. Kudhibiti na kuruhusu kisheria pombe ya kiasili. |
| 6 | Kupiga marufuku hatua za ushiriki umma zisizo bora na zenye kuendeshwa kwa hila ili kuhakikisha zimekuwa bora na yanaangazia maoni na utambuzi wa Wakenya na gharama yake inakubalika. | Kuwa na ofisi ya katibu/mwandishi wa Ushiriki Umma aliye na mamlaka ya kuendesha shughuli zote za ushiriki umma kwa niaba ya serikali katika viwango vya kitaifa na ugazuti. Kando na jukumu hili linalotarajiwa kuonyesha uwazi kwenye shughuli hii, afisi ipewe pia jukumu la kuhakikisha utetezi wa maslahi ya umma kwa njia ambayo inazuia ushawishi wa wafanyibiashara. Mfano mzuri upo katika moduli ya India. |
| 7 | Kwa kuunganishwa na ulinzi wa ushiriki wa umma, kupunguzwe jukumu lisilo na latili ya miundo msingi isiochaguliwa na watu binafsi wanaotumia nguvu za uchumi na hata ufisadi kutengeneza usimamizi wa serikali na uundaji wa sera kwa manufaa yao wenywe. | Sajili vikundi vyote vya ushawishi, na kuzidhibiti shughuli zao na mashirika ya umma, na mbinu zote za uundaji sheria kwenye afisi ya msimamizi wa ushiriki umma. |
| 8 | Zidisha uwezo wa watu wenye ulemavu kufikia majumba, sanasana ya umma, na usafiri wao | Weka wazi mbinu za kutekeleza sheria mwafaka kama njia ya mkataba wa kazi katika wizara, idara na wakala.<br>Tilia nguvu tume na makundi yaloanzishwa na mswada kuhusu watu wenye ulemavu. |
| 9. | Zidisha uhusiano na uelewa wa tofauti baina ya wakenya-sanasana baina ya wanafunzi-ili kutuwezesha sisi kuwa kwa pamoja | 1. Wizara ya elimu yafaa kuhakikisha shule za mabweni za umma na vyuo vikuu vina wanafunzi kutoka saehemu tofauti za nchi.<br>2. Juhudi za kipekee zafaa kubuniwa ili kujumuisha shule ili kuwepo jamii ambazo zimetambulikana kupigania raslimali kama maji na malisho-sanasana sehemu za kaskazini mwa nchi. |
| 10. | Zidisha u-pamoja katika serikali za majimbo/ugatuzi. | Kila hatua za kuzidisha u-pamoja katika viwango vya kitaifa zafaa kuonekana katika serikali za majimbo. |

**USTAWI WA PAMOJA**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Tunahitaji hatua kamili katika mtazamo wa uchumi wetu ili kukuza nafasi tosha za kazi kwa watu wetu walio na umri mdogo na kuifanya sehemu ya uchumi kubwa kiasi ili kutuletea kitenga uchumi kinachoweza kutuwezesha kuwahudumia watu na maslahi ya wananchi. | Kubali utaratibu wa kiuchumi (sio umiliki wa nchi) na uundaji bidhaa wenye kutumia kazi nyingi ya kuuza nchi za kigeni kwa eneo hili.<br>Fanya juhudi zote kuinua viwango vya akiba zaidi ya 25% ya GDP, na kukuza idadi za wafanyibiashara kwa kuhakikisha urahisi wa kufanya biashara kwa wanaoanzisha na biashara ndogondogo zimeongezewa mtawalia. |
| 2. | Mpango wa miaka 50 ya kujenga uchumi ambayo inatekeleza matakwa ya kizazi cha leo na kesho. | Mpango wa miaka 50 ambao ni wa kisiasa kuliko wenye ujuzi unaolenga kujumuisha Kenya na uchumi za dunia ambazo ni imara, dhabiti na zimefuzu. |
| 3 | Harakisha kujumuika kwa maeneo ili kuweza kufikia masoko na raslimali, kwa kuipatanisha eneo hilo na dunia nzima kama egemeo, ambalo litaiongoza kwa kukua kwa nguvu viwanda na nafasi za kazi. | Serikali yatakiwa kuharakisha jinsi ya utangamano kama hatua kuelekea ushirikisho wa kisiasa inapokubalika katika jumuiya ya jamii ya Afrika Mashariki. |
| 4 | Kubali mfumo wenye utazamo wa chini-juu ambao unaanza na sekta ya kilimo na wanyama wa nyumbani, kampuni za kiwango cha kijijini, sio fokasi ya juu-chini, na tuwe na fokasi na nia ya kuuangamiza ufisadi, kuiruhusu Kenya kupata “kasi za kuepuka” na iwe na uchumi wenye ushindi kamili wa kutupatia nafasi za kazi na kuinua mapato ya vitengo vingi. | 1. Nchi inafaa kufanya biashara ya kutengeneza masoko endelezi kwa kufungua masoko kwa dharura ya bidhaa za Kenya katika nchi jirani: na kuwapa habari husika wanaokuza bidhaa hapa Kenya kuhusu viwango vya thamani vinavyohitajika na ushindani wetu.<br>2. Kuwaletea karibu wafanyi biashara sehemu zinazopatikana bidhaa na zinazopeana ushauri kwa kinachotakiwa katika bidhaa na huduma, mchoro, kununua, na udhibiti wa hatua.<br>3. Jenga uchumi kutoka masahinani-mabadiliko kwa upangaji wa uchumi na sera zafaa kupatia nafasi zilizo rahisi sana kipao mbele katika uundaji bidhaa zinazohitaji nguvu mingi kikazi kama kilimo, mifugoi, na samaki, na kuikuza uwezo wa teknolojia wao kupitia kwa muda.<br>4. Pima idadi ya viwanda vya kijijini katika kilimo, na kile zinazoleta, na muwekeze katika kuzidisha idadi na kupanua zilizoko na zinazoendelea. Hii yafaa kuwa kipimo |

| | | |
|---|---|---|
| | | kamili cha uangalifu mwema wa uchumi na utaratibu wake.<br>5. Panua kilimo na ufugaji na huduma za mawaidha, ili kuhakikisha wosia wa kiustadi na kuunganisha masoko. Yanafaa kutuongoza katika utoaji wa bidhaa katika mashamba imeimarika sana kwa upeo.<br>6. Wezesha unyunyizi wa maji na kuiweka ufisadi kwa wanaoyangalia mambo na unyunyiziaji kama ajenda kuu katika juhudi za kuopambana na ufisadi.<br>7. Kuza viwanda mashambani bila ya kuangalia mbinu kaidi za kiteknolojia ili Kenya itumie mauzo ya bidhaa ya vitu hivyo na kuzibadilisha na bidhaa zenye uzito kama mashine, zinazoaweza kutumika katika utengenezaji wa bidhaa katika viwanda.<br>8. Pima idadi ya wafanyikazi wa kilimo na ufugaji na pesa wanayoingoza na kuundwa katika sekta hizo na kuwapa motisha wa kuzidisha kazi yao.<br>9. Endelea kupanua lami na barabara za maramu ili kuhakikisha wakuzaji bidhaa wote Kenya wamefikia masoko.<br>10. Hakikisha bei ya stima iko chini hakika na kimu chake kinaeza tegemewa ili kuwezesha biashara, na sanasansa wenye viwanda ili kushindana kidunia.<br>11. Wekeza na kukuza utafiti unaoiwezesha uzao na ushindani wa Kenya sanasana katika sdekta kilimo na ufugaji . |
| 6 | Akiba ni uwekezaji | 1. Anzia kazi kubwa ya kuinua akiba za kindani za nchi ifikie kwa aghalau 25% ya GDP kama Kenya itaweza kuwa na uwezo wa kusukuma uwekezaji katika vitengo mbalimbali, mojawepo ikiwa ni viwanda vyenye utumiaji wa kazi mingi ili kazin ipatikane kwa wakenya. Kunafaaa kuwa na ushuru na udhibioti wa motisha na mbinu za akiba ya elimu na ustaafu, na vitu nyingine za harambee ambazo wakenya wana habari watazilipia-kutoka mazishini hadi harusini, na hata ujenzi.<br>2. Ulipaji kutoka kwa wanaoishi mbali na sehermu zao za kuzaliwa-Enda mbele ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | kuwapendezea watu wakupe marupurupu, ulinzi na njia mwafaka ili kuwawezesha wakenya hao kuwa na akiba humu nchini. |
| 7. | Mishahara ya sekta ya umma | Tume ya mishahara na ujira yafaa kupanga upya mishahara yote bya sekta za umma nchini ili kuitatua swala nyeti ya mapato. |
| 8 | Kukopesha kwa sekta za kwanza muhimu | Serikali yafaa kutoa sera inayopeana mwelekeo wa kishedria na udhibitioshaji kwa benki kukopesha sehemu ya kutia hati ili kuipa kipao mbele sekta kama biashara ndogo, za wastani na zile ndogo kabisa, deni la mauzo la nje, uundaji bidhaa viwanda, ujenzi, elimu, afya, nguvu za kawi, usafi na uchafu kukadiriwa, na kilimo (inahusisha ufugaji na samaki). Benki kama zinakosa kujitwika kwa jambo moja,zitawezeshaw kupindua hela zake na kuzipaean katika benki ambayo ijmaweeza kuyatenda hayo majukumu. |
| 9.. | Imarisha ulinzi wa watumiaji bidhaa, sana sana kwa wakopaji | Kudhibiti kwa kiusawa ‘application’ za mtandao za mikopo ambazo zinawafanya wakenya kukaa kwa deni hadi kiwango haribifu kwa kuwa kiwango chao cha riba kimezidi na kukopa kutoka kwa wakopeshanaji. |
| 10. | Ujenzi wa viwanda yafaa iwe maana na simulizi ambayo inaongozaa serikali | Ujenzi wa viwanda pekee ndio utaiwezesha Kenya kuvuna talanta na maazimio ya kufikia ustawi wa kitaifa uliojimudu. Ni muhimu sana kwa wakemya na serikali kukataa kabisa dhana eti kuwa Kenya na nchi zingine za Afrika haziwezi fikia ujenzi wa viwanda sababu ya mwendo wa ubadilifu wa kiteknolojia kwa mfano, katika upeo wa utumiaji ya mashine zinaazofanya kazi kama mtu. Uadilifu wa mkoa hutupa nafasi nzuri ya kuinua utengenazaji bidhaa na ujenzi wa viwanda. Serikali yafaa kuifanya juhudi za kukuza ujenzi wa viwanda kuwa mada kuu na kuifanya iwe simulizi nzito kwa wananchi. Juhudi hizi zafaa kuwa zimesimamiwa na motisha na utaratibu ili kufikia teknolojia iliyo ya chini kikazi, Uzito wa ujenzi wa viwanda, ujenzi wa viwanda ulioongozwa na ufanyi biashara, na kuyainua matendo |

| | | |
|---|---|---|
| | | ya huduma na sekta ya ufumbuzi yenye kutengeneza bidhaa kawaida. |
| 11 | Linda uzinduzi wa Kenya, rasalimali jenetiki, ujuzi wa kitamaduni na maogezi kama dizaini za mali inayolindwa na sharia na sera. | Mtazamo wa keshon wa uzinduzi na uvumbuzi uko mikononi mwa utumizi wa mali kiakili, jenetiki, na vitu vyenye uhai wa ujuzi uliokarabatiwa na kizazi baada ya kingine katika jamii. Sheria za Kenya zafaa kuundwa ili kuwalinda haya raslimali kwa mkazo, na serikali kuundwa vyema ili kuinua kiwango cha kuridhisha duniani kote. Hii yafaa kuandamana na mifumo kwa maatumizi yanayozidisha uwezo wa wakenya kujijenga kwa mali hio. |
| 12 | Tahadhari na janga la ufisadi, kuundwa kwa muungano wa wakiritimba, na matumizi mabaya ya mamlaka ya kiuchumi katika uingizai bidhaa kutoka nchi za njeinayoweza kuleta bidhaa mbaya kwa bei ya juu. | Kuwa na mtazamo imara na uwekezaji katika kukuza uuzaji bidhaa katika nchi za nje, ambayo itahitaji kampuni na bidhaa kuwa na ushindani duniani, na hivyo nbasi kuwa na manufaa zaidi . |
| 13 | Kifungu ya 43 ya haki za uchumi na ushirikiano yafaa kutekelezwa ki-endelevu na makinifu na kila kiongozi aliyechaguliwa na manifesto za vyama vyao vya kisiasa. | 1. Serikali ya kitaifa na majimbo yafaa kubuni sera na viwango vya kuiongoza utekelezaji wa kifungu cha 43 cha uchumi na haki za kijamii.<br>2. Kifungu cha 43 cha Uchumi na haki za kijamii inapaswa kutekelezwa kwa kina na viongozi wote waliochaguliwa kupitia manifesto ya uchaguzi ya vyama vyao vya kisiasa. Hii itahitaji vyama vyote vya kisiasa kuunda maono na sera ya kutekeleza mswada wa haki za kibinadamu (inayohusu pia uchumi na haki za jamii) kama sehemu moja ya upigiaji debe manifesto zao katika uchaguzi. |
| 14. | Kila kizazi cha wakenya chafaa kuishi katikia mapato yao.na sio kuchukua deni inayotumika kwaq mamabo yasiyo na maniufaa yoyote na haiwaletei manufaa wazi katika ustawi wa kitaifa. | 1. Kunafaa kuwa kizuizi dhabiti kwa kiwango cha deni kinachofahamu hatari kwa ukuaji wa kiuchumi na ustawi wa kizazi cha kesho. BBI inaonelea ya kwamba upunguifu wa bajeti ya serikali haifai kuzidi 3% ya GDP na pia deni ya kitaifa hairuhusiwi kupita 45% ya GDP.<br>2. Anzisha hazina huru inayoruhusu akiba kwa wakati wa dharura ama mambo yasiyoepukika siku zijazo.<br>3. Katika kila hotuba ya kitaifa yua kila mwaka, rais anafaa kuelezea kiwango cha deni ikiwemo uhusiano wake na mapato ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | kiserikali, GDP, na desturi ndani ya ukopaji au ulipaji mwaka unaofuata. Yeye anafaa pia kuelezea wazi ni hatua zipi amezichukua ili kusawazisha bajeti kupitia uangalifu wa matumizi ya fedha na mapinduzi yanayochukuliwa ili kuyapeleka mashirika yenye hasara kufikia kiwango cha kuleta faida. |
| 15. | Zidisha matumizi ya fedha kwa maendeeleo kama kiwango cha mapato ya serikali ili kuinua bidhaa na huduma za umma kwa wakenya. | 1. Kwa kina, punguza matumizi ya fedha kwa mambo yanasojirudia-hasa mishahara, matembezi na anasa, marupurupu-kwa kupendelea utumizi wa hizo pesa kwa maendeleo.<br>2. Kunafaa kuwa elezo kamili ya mamlaka ya sheria na usimamizi wa tume ya mishahara na ujira ili kuhakikisha inasimamia kwa uangalifu mapenedekezo na mabadiliko ya mishahara yote.<br>3. Kuzivuta majumba ya uwezeshaji katika huduma za umma na matumizi ya teknolojia ili kuchukua hesabu ya zile hazitumiki (sanasana jumba za mikutano kabla kukodisha hoteli yoyote ile)<br>4. Kupiga marufuku matumizi mabaya ya gfedha-kwa mfano, hakuna, magari mapya au kupiga msasa afisi kwa mawaziri wanaoingia kazi au makatibu pasipo usimamizi na uangalizi.<br>5. Piga marufuku ulipaji wa marupurupu kwa wafanyikazi wa umma walio na mishahara.<br>6. Lenga uwiano, ulioandikwa kisheria, wa 70:30 kwa maendeleo ikilinganishawa na matumizi yanaojirudia.<br>7. Piga marufuku matumizi mabaya ya fedha katika serikali za kitaifa na za majimbo kwa kuleta sheria na kanuni zilizowekwa ili kupata hakikisho ya vitu kama magari mapya au kupigwa misasa kwa maofisi kwa maafisa wapya wanaoingia afisini kufuata njia mwafaka katika kupanga, bajeti na hata kukuwadia. |
| 16. | Twaa miradi iliyoruhusiwa na katiba na ya serikali amabyo inaagaziwa kwa maskini sana na wasiojiweza kwa wadi zinazohitimu kuchgaguliwa na sio kaunti, | 1. CRA ibadilishe kauli ya kuopeana mapato-sanasana kuzipean fedha kwa walioachwa kimaendeleo-ili kuashiria wadi ka tika bajeti za kaunti. |

| | | |
|---|---|---|
| | ili wale walioachwa nyuma wanaeza pata usiadizi kutoka kwa raslimali za kitaifa. | 2. Hakuna mkenya anayebaki nje- “Kubadili Plan” ya kuzileta wadi zilizotengwa kufikia kiwango cha kusherehekera pamoja na sehemu zingine za nchi.Jua hizo wadi ambazo zimetengwa kwelikweli, kwa sasa na jadi. Utekelezaji wafaa kuanzia kwa wadi zinazotokea mwisho. Zindua mpango wa kujenga mashule, vituo vya afya,barabara, maji, nguvu za umeme, na vituo vya polisi, na kuhakikisha vituo hivyo vimejengwa katika wadi zote katika muda wa miaka tatu. |
| 17 | Ruzuku yafaa kudhibitishwa uhalali na sio wa kudumu | Kando na sekta au mali inaotumiwa sana katika usalama wa wakenya, uwiano wa kitaifa, na uendelevu wan chi, serikali yafaa kupeana ruzuku wakati uwezo wa kustawisha iko nadra kupoatikanaa. Ambapo ruzuku imepeanwa, kunafaa kuwa matarajio yanaoeleweka, na yanaonekana kwa mpangilio rasmi wa hilo nakala, kuwa sekta hio inafanya kazi ili iwe na ushindani mwafaka ndio isitegemee ruzuku tena. |
| 18 | Kampuniu za kamari za kibinafsi zinachangia kukosa matarajio na umaskini mwingi | Kampuni la bahati nasibu la kiserikali lichukue nafasi ya kampuni za kibinafsi za kamari, ambao mapato kutoka kampuni hilo kama ilivyo desturi nchi nyiongine, yatumike kwa mambo ya kuwainua wanarika, michezo, tamaduni na mambo mengine ya kijamii yenye manufaa kwa wananchi. |
| 19. | Jukumu la weledi/wajuzi | Kongamano la wenye ujuzi na mikakati yao ya upatanisho na ukosoaji weledi yafaa kuongezewa nguvu juu ya dhana ya sharia na iletwe katika sura ya 6 yote. |
| 20. | Mafunzo ya maadili ya maisha na kuyatambua | Mtalaa wa elimu kutoka ya zamani hadi ya sasa ambayo iko imehitimu kiviwango inafaa haswa kuhusisha maadili na uraia kama kitangulizi katika mitihani na hata kufuzu shahada. |
| 21. | Andaa mipango maalum yenye husika na binadamu na usalama wa wakenya kama njia ya kupima utenda-kazi wa taifa, kaunti, na wadi | Bodi la utafiti na idadi ya watu Kenya yafaa kuvumbua kipimo ya ukuaji wa binadfamu ambayo inaidilisha mlengo wajumuiya ya nchi, UN, nainaifanya kuipanua kifungu 43 juu ya uchumi na haki |

| | | |
|---|---|---|
| | | za kijamii. Ripoti hioyo uyafaa kuchapishwa kila mwaka. |
| 22 | Punguza mikopo serikali inayochukua ili kufadhili matumizi ya juu ya kiserikali | 1. Kando na wakati wa majanga ya kitaifa ya dharura au vita, ambazo utangazwa rasmi-deni ya serikali yafaa sharti iwe (imepitishwa na kamati ya mawaziri na bajeti imefamnywa) kwa miradi ya maendeleo pekee.<br>2. Kunafaa kuwa dhamana na vikwazo kwa wale wanokiuka hii agizo. |
| 23. | Zidisha uwezo wa mipangilio ya elimu ili kujuwa na kuyajibu maswala ya mahitaji spesheli. | Tafuta na uwekeze katika talanta spesheli na mahitaji spesheli katika elimu ya awali ya watoto wadogo. |
| 24. | Pima usawa mahitaji ya ukuaji wa uchumi na hitaji ili kulinda mazingira na uwakilishaji wa wanyama na miti kwa kizazi kijacho. Pia, epuka laana ya mafuta na madini, vile vile kuzitaifisha raslimali,vilevile kuinua kiwangoi cha utajiri wa taifa, kaunti na mashinani kutoka kwa raslimamli za kiataifa. | 1. Patanisha na uunganishe sharia ya mazingira na viunga vyake katika uchimbaji madini na mafuta ya petroleum.<br>2. Husisha ukarabati wa kuzuia uharibifu wa mazingira, kilimo na sehemu zote kama uwekezajoi wan chi za kigeni kwa faida na kwa msaada.<br>3. Rahisisha na ueleze wazi jamii na raia kuhusu kufanya lolote lkile na wawekezaji,ikiwepo kuitumia afisi ya rapocha wa umma. |
| 25. | Kutoka kilimo kidogo cha nyumbani kufikia kulima mashamba makubwa ya biashara na ufugaji nwa mifugo, kupitia kuwealeta waklulima wapya wenye ujuzi. | 1. Futa jasho, tia motisha na uinue ujuzi wa vijana wadogo ili kukichukua kilimo na ufugaji mifugo wa kisasa kwa manufaa ya kibiashara.<br>2. Pendeleza unyunyizaji na ukulima wa sehemu zenye hali imekauka ya nhewa.<br>3. Mafundisho yenye mkazo na mengi kwa wakulima juu ya kukabiliana na hali ya kubadilika kwa hali ya nhewa. |
| 26. | Udhamini wa sekta ya kilimo yafaa kufuatwa na usaidizi mkubwa wa wakulima kwa mapito ya kuelekea mimea yenye faida na inayoiweza kukuzwa kwa kuhimili | Wakulima wanafaa kusaoidiwa ili wakuwe washindani na wenye mazao. Haswa, sekta ya kilimo na mimea inayohitaji kutiliwa sana rasilimali za umma zinafaa kuwa na mipango kamili ya mapito kwa mimea ingine yenye faida au yenye mazao tele. |
| 27 | Maliza ukiritimba na muungano wao katika sekta ya kilimoambao wanalazimishwa kutekelezwa kwa niaba ya wanaume-wa-katikati dhidi ya mapenzi ya wanaokuza bidhaa na wanaozitumia | 1. Kuza na zindua soko la bidhaa kwa bidhaa za kilimo.<br>2. Simamisha kuzuiliwa kwa biashara ya bidhaa za kilimokama kupigwa mnada kwa kahawa. |

| | | |
|---|---|---|
| 28 | Andaa mikakati yote ya kupunguza bei ya chakula kwa mkenya wa kawaida kwa kushawishi mazao ya hali ya juu kwa wahusika wote. | 1. Kuhimiza biashara ya kilimo kikubwa kwa masoko ya kimataifa na kiasi kidogo kiuzwe kwenye masoko ya nyumbani.<br>2. Kupunguza uharibifu wa chakula kwa kupatia sekta ya kibinafsi marupurupu |

| | | |
|---|---|---|
| 29 | Kusaidia wakulima na ukulima kwa kuhimiza malipo ya fedha /vocha papo hapo badala ya uhamishaji wa chakula wa moja kwa moja. Hili ni rahisi kutekeleza na inaboresha lishe na kusaidia wakulima | 1. MPESA husaidia kutuma na kupokea pesa kote nchini<br>2. Kuhimiza washirika wa misaada ya chakula ya kimataifa kutumia pesa taslimu na vocha, hili linaweza kuanza kutumika. |
| 30 | Kuongezea viwango vya usalama wa chakula nchini ili kuyafanya mazao yetu ya kilimo kuvutia katika masoko ya nje na hivyo kuongezea nafasi za ajira. | 1. Kusawazisha udhibiti wa minyororo ya uzalishaji wa chakula ili kuleta usalama na uwazi.<br>2. Kumrudisha afisa wa ugani wa kilimo kwenye kazi kwa upana |
| 31 | Kuongezea upatikanaji wa ardhi ya kuwekeza katika kilimo kwa vijana na wajasiriamali. | 1. Hakikisha kuna usalama wa kisheria ulio wazi na rahisi kwa mwenye ardhi, mjasiriamali, na mwekezaji.<br>2. Kumalizia kudijitalisha umiliki wa ardhi na kuwezesha umma kuifikia kwenye ‘database’<br>3. Kuramani na kuweka wazi kwa umma ardhi iliyomilikiwa na serikali ili kuikodisha kibiashara kwa masharti yanayoweza kufuatwa kwa urahisi. |
| 32 | Kuongezea ajira na maisha kwa kuzifanya biashara ndogo rahisi kushindana na kukua | 1. Kukuza na kuzindua kipimo cha kurahisisha kufanya biashara ndogo kwa wakenya bali sio wawekezaji wa nje<br>2. Kupunguza utozaji kodi wa biashara zinazoanza na zilendogo za angalau miaka saba kama njia ya kusaidia vijana katika biashara na kuwa na nafasi za ajira. |
| 33 | Kukuza ujasiriamali na ujuzi wa vijana wakiwa na umri mdogo ili waweze kujitegemea | 1. Kulazimisha sekta ya kibinafsi kuunda shirika la kitaifa isiyo ya faida, inayotoa ushauri, mafunzo na vifaa vya kuwasaidia vijana wanaotaka kufanya biashara wenye umri wa kati ya miaka 18-35. Rais awe ndiye mwenyekiti. Vijana hawa pia wapewe washauri wa maendeleo ya biashara.<br>2. Kutafuta vitengo vya utambuzi wa bidhaa vyenye uzoefu nje ya nchi vilivyo tayari kuanzisha maduka nchini ambayo yanaweza kusaidia wajasiriamali kuwa na |

| | | |
|---|---|---|
| | | maarifa zaidi na kuwashauri kuhusu kuzalisha bidhaa zenye ushindani katika masoko ya ndani nay a nje.<br>3. Unganisha ujasiriamali wa shirika hili na fedha za vijana za serikali.<br>4. Shirika hili litoe utayari wa kazi, ujasiriamali, na mafunzo ya kifedha, kwa kutumia watu anaojitolea, katika mashule kuanzia kwa umri wa miaka 12 hadi wakafuzu.<br>5. Mipango yote ya uwajibikaji wa mashirika ya kijamii ihamasishwe kujuimuisha kijenzi hiki. |
| 34 | Kupatia wakenya wote kiwango cha chini cha elimu kinachowawezesha kupata ajira au nafasi ya ujasiriamali | 1. Kuhakikisha kwamba uwekezaji na sheria katika elimu zinatolewa kwa kuzingatia idadi ya watu na ufikiji wa kijiografia.<br>2. Kukuza shule za kiufundi – katika umri wa ujana- kama njia mbadala katika njia ya kitaaluma.<br>3. Kufanikiwa kwa pamoja kunahitaji lishe sahihi na kuchochea watoto mara baada ya kuzaliwa. |
| 35 | Kuratibu mipango na maendeleo ya kitaifa na kaunti na kuhakikisha kuwa miradi ya kitaifa imetekelezwa, na maeneo yaliyoathirika zaidi yamenufaika. | Kuimarisha mashauri ya serikali ya kati katika kupanga miradi ya kitaifa. |
| 36 | Kugawia wasiojiweza ustawi wa nyumbani kwa kutambua kuwa kazi za nyumbani ni kazi pia zinazokubalika kisheria na huchangia sana kwenye kazi na thaman zinzafaa kuonyeshwa katika hatua zozote za kugawanyika au kutalikiana. | Kuweka wazi katika sharia ili kusanifu maamuzi ya korti kwenye mchango, muda wa ndoa, na sababu nyinginezo kama ilivyo kwnye mfumo wa Kadhi. |
| 37 | Kulinda watoto waliozaliwa nje ya ndoa | Kutekeleza sharia na masharti yanayofaa na kupewa kipaumbele |
| 38 | Kuchochea ili kuongezea utoaji wa hisani/hiari na kujitolea | Serikali (KRA) itumie msimbo wa ushuru kuchochea utoaji wa hisani na majukumu ya shirika la kijamii. |
| 39 | Weka mzigo wa ushuru kuwa kiwango cha chini ili kuwapatia wakenya nafasi ya kuchagua jinsi ya kutumia mapato yao kuliko serikali ambayo ina viwango vya juu vya utumiaji na uhamishaji mbaya | 1. Kuchukua hatua kali za kuzingatia mitazamo mipya ya kurahisiha ulipaji ushuru.<br>2. Kupunguza ukwepaji wa kodi na wafanyabiashara ili kuhakikisha kuwa mapato yanatosha wakati kodi ya jumla inatolewa. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 3. Kuadhibu ukwepaji wa kodi pamoja na wale wanaosaidia ukwepaji huo katika sekta ya kibinafsi na katika serikali. |
| 40 | Unganisha mishahara ya juu na ya chini katika Huduma ya Umma na kupunguza tofauti hizo | Kuweka mipaka kwa nyongeza ya mishahara kwa wafanyikazi walio kwenye sekta ya umma wanaopata zaidi ya shilingi laki mbili kwa mwezi. |
| 41 | Kuongeza uwajibikaji na utendakazi mzuri kwenye Huduma ya Umma | 1. Kuwaajiri makatibu wakuu kwa kutia mkataba ulio wazi na wenye vipimo vya utendakazi vinavyoweza kupimika na kufikiwa na umma.<br>2. Maafisa wenye vyeo vikubwa watathminiwe kwa kutumia alama za wazi zilizopigwa moto kutoka kwa wateule wa kisiasa na ambazo ziko wazi kwa mapitio ya baadaye na PSC kwa wale waliofukuzwa kazi. |

## Ugatuzi

| | Suluhisho | Hatua inayohitajika |
|---|---|---|
| 1 | Kwa kiasi kikubwa, wakenya wanafurahia ugatuzi na wangependa kaunti zote 47 zibaki. | Kuhifadhi hali ilivyo. Kwa kutegemea masauriano zaidi na wakenya, nivizuri uzingatie kwamba japo Wakenya wanaunga mkono ugatuzi nakaunti zao, wanataka thamani bora ya pesa na pesa zitumike katika maendeleo tofauti na kwenye gharama za kawaida na za kiutawala zilizo juu. |
| 2 | Utawala wa jinsia | Kugombea kiti cha ugavana na naibu wake kuzingatie jinsia, gavana awe wa kiume na naibu wake awe wa kike au kinyume chake. |
| 3 | Kujaza nafasi katika afisi ya naibu wa gavana | 1. Mwenzi wa mgombea kiti cha ugavana shharti awe wa jinsia tofauti.<br>2. Pale nafasi inapojitokeza kya naibu wa gavana, na gavana akose kumteua naibu katika kipindi cha siku tisini, spika wa bunge kwa idhini ya bunge atateua naibu wa gavana. |
| 4 | Usimamizi wa matumizi uwekezaji, na uajiri wa kaunti haukufanikiwa katika viwango vingi na umeleta matumizi mabaya na pia ufisadi zinazokandamiza ugatuzi na imekuwa kama kawaida kwa | 1. Urari wa matumizi ya fedha kati ya mara kwa mara nay a maendeleo uwe kama ule wa serikali ya kitaifa; 70:30<br>2. Kuweka mipaka ya wanaoajiriw kwenye kaunti kwa kuzingatia idadi ya watu nan a idadi ya waajiriwa. |

| | | |
|---|---|---|
| | Wakenya. Dawa yake ni kuwa na usimamizi mkali sana ufanywao na mashirika mahususi. | 3. Kuimarisha hali ya kujitegemea ya usimamizi wa bunge la kaunti kwa kuhakikisha uongozi wa bajeti za bunge hiyo zimejihami dhidi ya kuingiliwa kisiasa au kiholela na upande wa utendaji wa kaunti; hatua hizi zinafaa kufuata michakato ya usimamizi wa fedha za umma.<br>4. Kuna akiba ubwa katika kuondoa urudufu wa kazi kati ya serikali kuu nay a kaunti.<br>5. Kuboresha kazi kwenye serikali za kaunti: nyingi zina wafanyikazi zaidi wanavyohitajika.<br>6. Ili kumaliza tabia ya miradi kutokamilishwa, palipo na mabadiliko ya utawala, Hazina haitofaa kuachilia pesa kwa gavana mpya kabla ya kupata orodha ya miradi ambayo haijakamilika na mpango alionao wa kuikamilisha. Iwapo hana mpango wowote na wala hataki kuikamilisha, awasilishe taarifa yenye maelezo kamili kisheria.<br>7. Usimamizi wa miradi inayoanzishwa katika mwaka wa mwisho kabla ya kupiga kura tena uchunguzwe kwa undani na mdhibiti wa bajeti, bunge la kaunti seneti na mamlaka yote ya usimamizi.<br>8. Kuimarisha mifumo ya kifedha kwenye serikali za kaunti na kuweka matumizi na bajeti kwenye mitandao.<br>9. Kuimarisha afisi ya Mkaguzi Mkuu ambayo inafaa kugatuliwa ili kusimamia akaunti za kaunti na kutoa ripoti yake kwa njia wazi iayofikika.<br>10. Pesa ziachiliwe na Mdhibiti wa Bajeti baada ya kutathminiwa na kuthibitishwa kwamba zilizotumwa awali zimetumika ipasavyo.<br>11. Kila mradi wa maendeleo unafaa kuwa na kibao kinachotoa maelezo yake, mwenye kandarasi, na nambari za simu ili wakenya waweze kutoa taarifa iwapo watagundua kasoro yoyote katika utekelezaji wake. |
| 5 | Fanya ajira za kaunti kuwa na ujumuishi zaidi, zenye kuzingatia misingi ya sifa zinazohitajika na inayolenga utendakazi. | Jinsi PSC inavyojitegemea, vivyo hivyo idhihirike kwenye kaunti. Jukumu hilo iwe na wajibu wa kuajiri wafanyikazi wapya kuweka viwango vya ulipaji vinavyolingana na vya serikali ya kitaifa huku ikihakikisha ujumuishi na ikijenga uwezo na ujuzi wa walioajiriwa. |
| 6 | Kuhakikisha pesa ya maendeleo imebajetiwa ili kushughulikiamahitaji maalum kwenye wadi badala ya | 1. Kuunda na kupitisha sharia kuhusu uundaji wa kambi za kaunti, misaada yenye masharti, na ufadhili na uwekezaji wa wafadhili wa kigeni. |

| | | |
|---|---|---|
| | kaunti au maeneo bunge kupewa pesa nyingi. | 2. Kuzingatia jinsi wawakilishi wa wadi wanaweza kusimamia fedha za basari tu huku wakihakikisha pesa za maendeleo ya kaunti (CDF) hazigongani na maendeleo ya lazima ya kaunti.<br>3. CRA ibadilishe mgao wao wa mapato haswa katika kugawa pesa kwa wasiojiweza ilikulenga wadi kwenye bajeti za kaunti.<br>4. Shirika l Kitaifa la Takwimu itoe lengo na kipimo cha ndani cha ustawi na usalama wa binadamu, pamoja na uendelevu wa mazingira ya wakenya kama njia ya kupima utendaji wa kitaifa, kaunti na wadi.<br>5. Misaada yenye masharti inaweza kutumika kutia kaunti moyo na pia uudaji wa kambi zinazoboresha utoajo na upangaji wa maendeleo. |
| 7 | Boresha sera na taratibu zinazosaidia kaunti kukuza uchumi wao | 1. Kanuni za serikali ya kaunti na ukusanyaji wa mapato usigongane na motisha ya uwekezaji na uzinduzi.<br>2. Kila kaunti kuanzisha na kuweka kwa umma kanuni ya ujasiriamali na uwekezaji inayotekeleza katika njia bora na inayoweza kutabirika.<br>3. Biashara mashinani – kaunti zihakikishe makundi kwenye maeneo ya ndani yameanza biashara kwa kushirikiana na kuhakikisha imekuwa rahisi hata kwao kuziendeleza, kujifunza na kuunganika na masoko.<br>4. Kudijitalisha ukusanyaji wa mapato ili kuzuia wizi mdogo mdogo.<br>5. Weka mkanda mwekundu kwa kiwango cha chini kwa kufahamu kwamba wanashindana na kaunti na nchi nyingine.<br>6. Pasiwe na kutoa ushuru mara mbili au kanuni mara mbili kwenye viwango vya kitaifa na kaunti. |
| 8 | Kulazimisha utunzaji wa mazingira endelevu wa uchimbaji madini na unyonyaji wa mafuta unaotabirika, unaofaa kisheria na mzuri kibiashara ili kuongeza ustawi katika kaunti. | Makubaliano ya kweli, sera na kanuni katika madini na mafuta inapaswa kufanywa kwa umma katika njia inayopatikana, pamoja na uhasibu wazi wa ushiriki wa umma na tathmini ya athari za mazingira |
| 9 | Kufafanua, kunakili gharama na kuhamisha fedha kulingana na kazi za kitaifa na kata. | 1. Ni sharti tumalizie kwa haraka uhamishaji wa majukumu kutoka kwa serikali kuu hadi ya kaunti mara moja tu.<br>2. Mara tu majukumu haya yanapoletwa kwenye serikali ya kaunti, nashirika yasiyo yakiserikali |

| | | |
|---|---|---|
| | | yanayofanya kazi za kaunti yanafaa kuundwa upya.<br>3. Pesa hufuata majukumu. Tunahitaji kukamilisha gharama ya kazi za kitaifa na kaunti. Hivyo kunaeza kuwa na nyongeza katika ugawaji wa fedha kwenye kaunti. Waliozungumza na jopokazi walipendekeza kaunti zipate kati ya asilimia 35 na 50 ya mapato ya serikali ya kitaifa.<br>4. Hatua ya ugawaji inafaa kuwa rahisi sana kwa wananchi kuelewa na iongozwe na kanuni za kikatiiba kwa kuzingatia usawa na mahitaji ya kipekee.<br>5. Nyongeza ya pesa katika kaunti ongozwe na ugawaji wa mapato unaozingatia idadi ya watu; afya, ambayo inahitajika sana na wakenya wote, kilimo, na utoaji huduma na wala sio ukubwa wa ardhi na vile vile kwa kuangalia ubaguzi uliokuwapo na uliopo.<br>6. Kila wadi ipate faida ya angalau asilimia 30 ya fedha ya maendeleo katika kila kipindi cha miaka mitano.<br>7. Weka wazi na kusimamia vyema fedha zinazozalishwa na kaunti.<br>8. Kutengeneza kichocheo kwa kizazi kilicho na uwazi katika raslimali za kaunti kwa kutoa pesa zaidi kutoka kwa vifaa vya kitaifa vilivyounganishwa na hii.<br>9. CRA kuchunguza kiwango ambacho kaunti zinafaa kuwa zikikusanya na kuiwekwa katika mgao wao wa kila mwaka.<br>10.CIDPs zafaa kuunganishwa na uchunguzi ulio wazi wa mahitaji ya maendeleo katika kila wadi.<br>11.Kata ushuru kulingana na mhasibu mkuu wa mahesabu ya kiserikali-Ni heri pesa ibakie kwenye mifuko ya wakenya mpaka kuwe na uhasibu na usimamizi wa matumizi yake,katika ngazi za kitaifa na hata kaunti.Kisha ushuru upandishwe na utenda kazi wao. |
| 11 | Kuimarisha mazungumzo na mshikamano wa kijamii katika kaunti,hususan kaunti ambazo zina makabila mengi kwa lengo la kuhakikisha kuwa jamii zenye idadi ndogo ya watu zinasikika na kuheshimiwa | 1. Uagaziaji zaidi wa kimila na heshima ya kuandaa na serikali za kaunti.<br>2. Chukua hatua za kuhakikisha mashule katika kaunti yanajumuishwa kikabila na kidini<br>3. Miradi ya maendeleo iliyogawa na miradi ya mazungumzo na jamii ambazo zimekuwa na historia ya mizozo. |

| | | |
|---|---|---|
| 12 | Wakenya wanahitaji huduma za afya njema kabisa ikiwa nchi hii itaweza kuwa na mazao na kuendelea mbele.Kulipia huduma za afya inakula sana akiba za kifamilia na hata saa zingine hulazimu kuuza sehemu za ardhi,amabayo kwa saa zingine huleta mzozo siku za usoni. | 1. Pendekezo za katiba kuhusu afya hazizingatiwi kikamilifu.<br>2. Majukumu ya afya yafaa kubakia na serikali za kaunti na fehda ziteremshwe juu ya jukumu hilo.<br>3. Tunahitaji agazo lenye nguvu sana kuhusiana na afya ya kimsingi na ile zulilifu.<br>4. Wakenya wanahitaji kipengee cha uhuru wa wagonjwa kukabiliana na maswala yafuatayo;Ulipaji umejawa na ufisadi na uongezeko wa pesa wakati wakenya hawajiwezi.Hakuna hospitali ina ruhusa ya kuwazuia wagonjwa cha lazima pasipo na pesa.Kunafaa kuwa na adhabu kali kwa vipimo vyenye makosa.Vituo vyote vyafaa kuwa na visa vya dharura dhabiti.Wagonjwa wote wanafaa kuogeleshwa kwa upole na kupata huduma inayostahili. |
| 13 | Hatutafaulu kupata huduma za afya safi kama usimamizi wa afya utakuwa ghali mno na kiwango cha ufisadi kibakie kuwa juu pia. | Gharama za usimamizi wa Bima ya Afya (NHIF) zinapaswa kupunguzwa zaidi kwa kutumia teknolojia,kupunguza visa vya ufisadi na kuongeza tija.Gharama hizi za kiusimamizi zinapaswa kuwa kati ya 55  na 10%. |

## Ufisadi

| | **Suluhisho** | **Hatua inayohitajika** |
|---|---|---|
| 1 | Kurudisha hadhi ya huduma ya umma kwa kupunguza migogoro ya ihasidi, ujihisishaji kwenye biashara na kuongezea uwazi na kuzuru kwingineko ilikujifundisha kuhusu utendakazi. | 1. Kuhusisha mafunzo ya uadilifu na tathmini ya utendakazi kwenye kila kozi ya huduma ya umma inayohitaika kwa kupandishwa cheo au kuhamishwa kikazi.<br>2. Kuanzisha mbinu za ufichuzi/upulizaji kipenga kwa wafanyikazi wa umma.<br>3. Mikataba yote ya wateuliwa wa vyeo vya juu iwe wazi kuhusu utendakazi pamoja na sheria za kuachishwa kazi iwapo mtu atashindwa kutenda kazi. Pia, kupitia mikataba yote ya maafisa wakubwa kila kati ya mwaka na kuwaachisha kazi wasio na rekodi nzuri ya kazi na wenye kuhusishwa na ufisadi.<br>4. Afisa wa serikali asifanye biashara yoyote na serikali.<br>5. Mke au mume wa mfanyikazi wa serikali asifanye biashara yoyote na serikali lakini anaweza kuifanya katika sekta ya kibinafsi. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 6. Ili kujihusisha na biashara nje ya serikali baada ya masaa ya kazi, mfanyikazi wa serikali anafaa kupata kibali kutoka kwa msimamizi wake kazini. Kibali hiki kitadhihirisha kuwa kazi au biashara hiyo haijazuiliwa kisheria, haimzuii afisa kutenda kazi yake na wala haiharibu hadhi ya huduma ya umma.<br>7. Afisa wa serikali atahitajika kuwasilisha ripoti iliyoandikwa kwa Tume mpya ya Maadili na Uadilifu kuonyesha hitaji la kifedha au nyinginezo aliyenalo yeye, mke/mume wake au mshiriki wake kisheria, mtoto au mzazi katika maamuzi ya MDA alikoajiriwa au katika serikali.<br>8. Mke/mume, mtoto, au mzazi wa mfanyikazi wa serikali atawasilisha ripoti iliyandikwa kwa Tume ya Maadili kuhusu mahitaji ya kifedha au mengineyo aliyonayo kwenye MDA iliyoajiri huyo Afisa.<br>9. Afisa wa umma atawasilisha taarifa iliyoandikwa kwa msimamizi wa mkuu wa hisa au kifedha na riba nyinginezo katika kampuni zinazohusiana na shirika lililomuajiri.<br>10. Maafisa wakuu wa umma wanaowakilisha serial kwenye bodi za kampuni za kibinafsi waeleze kwa uwazi ushawishi wowote unaowez kuleta mgogoro kwenye masuala yanayozungumziwa.<br>11. Afisa wa umma hataweza kutoa maamuzi au kushiriki katika maamuzi yanayoathiri ushawishi wa kifedha au mengineyo kuhusu;<br>• Mke/mume wake au mshiriki wake wa kisheria, mtoto, au mzazi.<br>• Watu binafsi au wanasheria aliojihusisha nao kwa kipindi kilichopita vha miaka mitano.<br>• Watu binafsi au wanasheriawaliomfadhili katika uchaguzi wake katika kipindi cha miaka mitano kilichopita.<br>• Makampuni au taasisi ambako afisa huyu anatarajia kuwa mwajiriwa.<br>• Mtu binafsi au mwanasheria ambaye yeye, mke/mume wake, mtoto, au |

| | | |
|---|---|---|
| | | mzazi wake wanahusika katika shughuli za kisheria au wanaodaiana. |
| 2 | Jukumu kwa kujiuzulu | Viongozi wanahitaji kuwa na jukumu la kisiasa kwa vitendo visivyopendeza vya serikali vinavyosababisha majanga hatari kwa kujiuzulu ii kuwepo na hatua ya kutafta njia mwafaka ya kuendesha usimamizi ufaao. Viongozi waelewe kuwa kujiuzulu sio tu njia bora pale palipo na utekelezaji wa majukumu tu bali pia ni njia ya kuonyesha heshima kwa wakenya na huashiiria uwajibikaji. |
| 3 | Uwajibikaji katika uongozi | Mojawapo ya sifa za kuwa katibu mkuu au mwanabaraza wa mawaziri hata kwenye kaunti ni kuwa tayari kuhusika kuleta mafanikio kwa kutumia huduma zilizopo na kuziendeleza kwa niaba ya wakenya. Iwapo mkenya atatumia na kufaidika na huduma hizo, afisa huyu pia zinamfaa. Watoto wa mawaziri watumie huduma hizo zilizopo kama vile, elimu, matibabu na mawaziri wote wa serikali kuu na kaunti wazitumie pia. |
| 4 | Uchunguzi na uendelezaji wa kesi wenye nguvu. | 1. Kuimarisha afisi za DPP na DCi kila wakati.<br>2. Shirika la kuokoa mali lihamishwe hadi kwa afisi ya DPP ili kuwe na usimamizi bora wakuokoa mali kutoka kwa magaidi watuhumiwa. |
| 5 | Benki zinazosaidia ufisadi ziwajibishwe. | 1. Benki inayohusika kwenye hatua za kifisadi za pesa ilipe pesa zote zilizopitishwa kwake pamoja riba.<br>2. Wote wanohusika katika utumaji na utoaji wa fedha za kifisadi pamoja wanaowalinda wanafaa kushtakiwa na kutozwa faii huku wakilipa fedha na mali yote iliyopitishwa kwenye benki hiyo pamoja na faini ambayo ni asilimia ya fedha zilizotumika.<br>3. Afisa mkuu wa benki anafaa kutozwa faini pia huu akilipa mali yote au sehemu ya mali hiyo iliyopondwa na kupitishwa kwenye benki yao na kutozwa faini pia, na kufungwa bila nafasi ya faini ya kutoenda jela.<br>4. Benki zinazopatikana na ufisadi mfululizo zipokonywe leseni zao za kazi. |
| 6. | Fedha za umma zilizotumiwa kama udhamini au ruzuku ziambatane na madhara ya uhalifu na ufisadi na kuwe | 1. Dhamini za dharura za vitengo vya sekta ya kibinafsi zenye hisa za serikali zinazotumia rasilmali za umma ziambatane na mabadiliko |

| | | |
|---|---|---|
| | na mipango wazi ya kuzirudisha zikiwa na faida. | makali yaonekanayo ambayo ni pamoja na uchunguzi wa kifedha, wa malipo yaliyofanywa ya kiutendaji, wa tabia za kimaisha, mabadiliko ya usimamizi na mpango ullio natarehe ya kurudisha /kuokoa mali na fedha za umma.<br>2. Kama Rais alivyoamuru Novemba 2015, mashirika yasiyo ya kiserikali yatengezwe kwa kuwa na malengo mapya kwenye kiini kikuu cha biashara na pia kupunguza uharibifu huku maadili yakizingatiwa.<br>3. Kuhimiza ubinafsishaji wa hisa za serikali ktika mali isiyoleta faida kwa umma na kuchukua muundo wa mashirika.<br>4. Pale ruzuku inapotolewa,  pawe na matarajio yenye faida yanayojionyesha katika stakabadhi rasmi ya mipango kwamba sekta hiyo inajikakamua kutohitaji ruzuku tena. |
| 7 | Kanuni za maadili mema kwa viongozi | Kuhakikisha viongozi wana maadili ya hali ya juu kwa kuweka mikakati ya kisheria na kanuni za madili mema ambayo ni pamoja na ufichuzi wa kifedha. Mawaziri wote,makatibu wakuu, na wagombea wa kiti cha ugavana watafuata kanuni za maadili pamoja na kusema wazi utajiri wao, hatua za kuweka wazi fedha zilizochapishw na kusikizwa katika bunge kabla ya uteuzi wao. |
| 8 | Kupeana kifuta jasho kwa habari zinazoelekea kufuzu kwa utekaji wa mali na kushtakiwa kwa wafisadi. | Kutoa asilimia tano ya mali iyiyopatikana kutoka kwa mashtaka ya ufisadi na kumpa aliyetoa taarifa kuihusu mali hiyo na mshtakiwa na iwe siri kwa kuzingatia usalama wa mtu huyo. |
| 9 | Uongozi wa utendakazi wa kitaifa na kaunti ufuate ufichuzi wa fedha ya umma. Hawa ni pamoja na rais, mawaziri, magavan, makatibu wakuu, afisa wakuu na wenyekiti wa mashirika yasiyo ya kiserikali na makampuni yenye hisa za serikali ya Kenya. | Kuweka wazi kwa umma hisa, ajira, amana za familia na za biashara, majumba, kandarasi za serikali, ukurugenzi uliosajiliwa, ubia, madeni, dhamana, uwekezaji, akaunti za kuwekeza, mali yoyote yenye thamani ya  zaidi ya milioni kumi, pahali pengine popote anapotoa mtu mapato, zawadi zenye thamani ya zaidi ya elfu hamsini (50,000) akiwa kazini, usafiri uliofadhiliwa na vitengo visivyo vya kiserikali, na uanachama wa mashirika yoyote yanayoweza ushawishi uletao mgogoro. |
| 10 | Kuzuia ukandamizwaji wa kisheria na maafisa wa umma,  wa wafichuzi wa habari  na wanahabari wanoripoti | Kurekebisha Sheria ya Kuharibu Jina ili kuzuia maafisa wa umma kuchukua hatua pale |

| | | |
|---|---|---|
| | kuhusu ufisadi na wizi wa pesa wa akili. | ambapo amepatikana na hatia, kuhusu masuala ya madili na ufisadi. |
| 11 | Kuongeza mahakama imani. | 1. Kuongeza imani ya umma kwenye mahakama kwa kutambua kuwa kanuni kuu za katiba nchini ni ugavi wa mamlaka kati ya mikono ya serikali na uwajibikaji kwa wanainchi. Hali ya mahakama kuwa inayoweza kujisimamia ilindwe kama kanuni kuu ila iwe pia inaweza kuwajibika kwa wakenya.<br>2. Kuwe na nafasi ya kipekee ya majaji na mahakimu watakaoshughulika na kesi za ugaidi, madawa ya kulevya, ufisadi na makosa mengine ya kigaidi na wawe na usalama wa kipekee unaotolewa na nchi/taifa.<br>3. Uwezo wa tume ya huduma za mahakama wa kuadhibu majaji ufanywe mpana ili tume hii iweze kuhudumia kisheria kamosa madogo madogo ya kitabia ya majaji yanayoathiri hadhi ya haki inayotolewa bila kuelekea hatua za kikatiba za kumwondoa afisini.<br>4. Imani ya watu kwa mahakama inahitaji watu kuamini jinsi mashtaka dhidi ya wafanyikazi wa mahakamani yanavyoendeshwa. Ili kuimarisha hatua za kushughulikia mashtaka mahakamani, afisi ya mtetezi wa wanamahakama inahitaji kupigwa jeki ili iweze kufikika  na umma. |
| 12 | Hatua zichukuliwe  li kuzuia matumizi mabaya ya shughuli za korti ya kukawisha na kukandamiza haki haswa pale watu wakubwa wanahusishwa na ufisadi. | Kupunguza muda unaotolewa ili kukamilisha kesi zinahosiana na uchumi na ufisadi. |
| 13 | Kutekeleza ukaguzi wa kujitegemea na mkali wa matumizi ya umma ili kuhakikisha inateka thamani ya pesa. | Hatua za ukaguzi ziwe na thamani na mkaguzi mkuu awasilishe kwenye bunge aina zifuatazo za ukaguzi:<br>• Ukaguzi wa kifedha wa akaunti zote za serikali ya kati huku **maoni yake yakitolewa kwa njia mbili** kuhusu akaunti hizo. Ya kwanza ikiwa ni iwapo akaunti hizo zinatoa mtazamo wa kweli na haki huku ya pili yakiwa ni kuhusu udhibiti, yaani kama fedha ziliidhinishwa na idara kutumiwa kama inavyodhihirika. |

| | | |
|---|---|---|
| | | • Aina nyingine ya ukaguzi inafaa kuonyesha thamani ya pesa kwa kupima uchumi, na ubora wa matumizi ya rasilmali za umma. Hii aina inafaakuonyesha iwapo rasilmali zilitumiwa vibaya kwa kununua vifaa visivyohitajika au la. |
| 14 | Afisi ya Mkaguzi mkuu kuongeza uwezo wa kufikia kaunti. | Kugatua afisi ya Mkaguzi mkuu hadi kwenye kaunti. |
| 15 | Kuimarisha usimamizi wa fedha za umma kwa kuiongezea kwenye afisi ya Mkaguzi mkuu. | 1. Kuboresha usimamizi wa manunuzi ya matumizi umma.<br>2. Kuboresha ukaguzi wa kabla ya matumizi. |
| 16. | Kuongezea uchunguzi wa mfumo wa manunuzi ya umma na wafanyakazi wake na kuhakikisha ukaguzi wa mara kwa mara. | Afisa wa manunuzi asiwe kwenye nafasi moja kwa zaidi ya miaka miwili. |
| 17. | Kuimarisha uwezo wa mdhibiti wa bajeti ili awe na uwezo wa kutambua na kushughulikia matumizi mabaya ya fedha na hatua zisizokubalika kisheria kwa wakati ufaao. | 1. Hatua zinazotumia teknolojia na mishakati ya haraka iwekwe ili kufuatilia namkutoa majibu ya haraka ya kusimamisha fedha za umma zinazogawanywa kwa njia isiyofaa.<br>2. kuautomatisha mifumo yote ya malipo ya serikali. |
| 18 | Kufanya Kenya kuwa taifa ya kutoa huduma kielektroniki kwa asilimia, kwa kuzifanya huduma zote, hatua, mifumo ya malipo na uwekaji rekodi za serikali wa kidijitali., | 1. Haya ni pamoja na kuwapatia wakenya vitambulisho vya kidijitali na rekodi na maelezo ya afya ya kielektroniki.<br>2. Wakenya waweze kupiga kura kielektroniki. |
| 19 | Kama Rais alivyoamuru Novemba 2015, mashirika yasiyo ya kiserikali yatengezwe kwa kuwa na malengo mapya kwenye kiini kikuu cha biashara na pia kupunguza uharibifu huku maadili yakizingatiwa. | Kutengeneza sharia ya kubadili mashirika yasiyo ya kiserikali na kuhakiki sheroa zilizopo ili kuhakikisha mfungamano. |
| 20 | Mtalaa wa elimu uongeze vipengele vya maadili na uraia kama hitaji muhimu kwenye mitihani na kufuzu kwao, kutoka kwenye kiwango cha chini hadi cha juu kabisa cha elimu. | Wizara ya elimu, na taasisi nyinginezo, za kibinafsi au za umma, zinazotoa mafundisho /elimu kwa wanafunzi, wawe wanarika au wazee, zinafaa kufuata muundo huu. |
| 21 | Maafisa wakuu hawafai kutumia fedha za umma kujifurahisha. | Bajeti za kuunda upya afisi, katika kila tawi la kiserikali zinafaa kuwasilishwa katika bunge angalau mara moja kwa kila miaka mitatu. |
| 22 | Kupunguza uharibifu unaoshuhudiwa kwenye umma unaofanya vifaa na magari ya serikali kuachwa bila kutumika. | Bajeti zote za ununuzi ziwekwe kipengele cha kuzikimu. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Kuboresha usimamizi wa utupaji wa mali ya serikali na kuunda kamati maalum ya utupaji wa mali inayohitaji kutupwa. |
| 23 | Kama Rais alivyoamuru Novemba 2015, sawazisha bei za serikali za zile za soko. | Mamlaka ya usimamizi wa manunuzi ya umma ichapishe kwa upana orodha ya marejeleo ya bei ya huduma na bidhaa. |
| 24 | Kuadhibu wale wanaoepuka kulipa kodi pamoja na wanaowasaidia kuepuka walio kwenye sekta za kibinafsi na kwenye serikali. | Washirika wa kihasibu na kisheria, Mamlaka ya Mapato, na vitengo vinginevyo vya kiserikali, pamoja na wafanyikazi wake, waweze kutozwa faini kali kwa kuwezesha uepukaji wa kulipa kodi wa watu binafsi au biashara. |
| 25 | Kutambua na kupunguza vifuta jasho katika huduma za umma zinazoendeleza ufisadi, ulinzi kwenye milango, na utafutaji wa ada za nyumba.<br>Kuondoa marupurupu ya usafiri. | Kufanya ukaguzi wa hali ya juu wa marupurupu hasi ya kisheria, sera na utawala kwenye huduma za umma yanayokandamiza thamani ya fedha, haki na ubora wa huduma za umma. Matokeo yake yaunde sera nayatekelezwe. |
| 26 | Kando na kuwaadhibu wafisadi kwa kuwaweka jela, walioibia wakenya wahakikishwe kuwa hawana nafasi tena kwenye uongozi, kwenye huduma za umma au hawafanyi biashara na serikali. | Kuwataja na kuwaaibisha washtakiwa wa ufisadi kwa kuweka wazi mali iliookolewa na kuwataja majina yao kwenye umma. Wanaoshtakiwa waondolewe kwenye kuhudumia umma na wazuiwe kufanya biashara na serikali. |
| 27 | Kuepuka biashara kubwa zinazoweza kufeli ambazo zitahitaji kudhaminiwa na rasilmali za umma. | Pale kampuni za aina hii zinapokuwepo kwa muda Fulani, ziwe chini ya utawala mkali wa kiserikali. |
| 28 | Kuhakikisha hakuna vitengo vya sekta ya kibinafsi vilivyo vikubwa vinavyofurahia ukiritimba na ambavyo kuanguka kwake kunaweza kusababisha maafa ya kitaifa. | Kuimarisha uwezo wa kujitegemea kwa mamlaka ya ushindani ili kupunguza ukuaji huu kuwa mkubwa-unaoweza-kufeli. |
| 29 | Mpango wa kitaifa ulio wazi unaowasilisha mabadiliko ya sekta ya umma na mfumo wa kaunti ulionyooka. Hili litaweza kuhitaji mpango wa maagizo wenye mkakati wazi wa mawasiliano na kisiasa. | 1. Kuondoa kurudufu kwa majukumu ya kazi kwenye viwango vya kitaifa na kaunti ili kuleta matumizi ya pesa yaliyopungua.<br>2. Kusawazisha malipo ya serikali ya kaunti na ya kitaifa<br>3. Kutumia "uharibifu wa kiasili" na kuondoa ajira ili kupunguza ukubwa wa huduma ya umma. |
| 30 | Kuhakikisha viongozi wana maadili ya hali ya juu kwa kuweka mikakati ya kisheria na kanuni za madili mema ambayo ni pamoja na ufichuzi wa kifedha. | Mawaziri wote,makatibu wakuu, na wagombea wa kiti cha ugavana watafuata kanuni za maadili pamoja na kusema wazi utajiri wao, hatua za kuweka wazi fedha zilizochapishw na kusikizwa katika bunge kabla ya uteuzi wao |

| | | |
|---|---|---|
| 31 | Kuunganisha mifumo ya kitamaduni na kijamii zinazotuza au kuondoa heshima ya mtu na familia kwenye vita dhidi ya ufisadi. | 1. Kuhakikisha kuwa wazee wote nchini wanaoendesha sherehe za jandoni kwa wanarika wamefundisha haja ya kuwa waadilifu. – kwamba waitunze Kenya kila siku kwa kupendana ka kupinga ufisadi.<br>2. Kupanga kongamano la mwungano wa uongozi kwenye kiunzi cha uadilifu katika kukubali wanachama wapya. Wale wanaohusika na matumizi mabaya ya ofisi na ufisadi wasikubaliwe kwenye mwungano huo. |
| 32. | Dini ilindwe kutokana na ufisadi na wizi wa fedha wa kiakili. | 1. Mkuu wa sharia apange kongamano koja kuu ya makanisa, misikiti, mahekalu na dini zingine na washikadau ili kujadiliana na kukubaliana kuhusu mhimili wa kisheria, uliochukuliwa kwenye sharia ambao utaokoa dini kutokana na ufisadi na wizi wa fedha huku ukiboresha utawala.<br>2. Kuhakikisha kuna waziri ambaye anashughulikia masuala ya dini kwa ukamilifu. |
| 33 | Michakato ya muungano wa wenye ujuzi kwa mazungumzo na kusuta kwenye ujuzi yafaa kutiliwa nguvu upya kama ipasavyo kisheraina ilivyoletwa katika kipengee chote cha 6. | Wenye ujuzi wanafaa kuwa wamekinziwa kisheria na uwazi na uwajibikaji wa kiumma na mbinu za adhibu kwa wanachama ambao ugandamiza juhudi na viwango vya kisheria. |
| 34 | Shukisha hamu ya kusaka pesa kupitia kwa ufisadi ili kusababisha maisha ya kustaafu.Maafisa wanaopitia maisha ya kibinafsi kutoka maisha ya huduma ya umma wanafaa kupewa sapoti mingi ili kuwawezesha kupata miradi na ajira. | 1.Sekta ya kibinafsi yafaa kupewa jukumu la kuanzisha kikundi cha kujitolea mabacho kinanuia kusababisha ajira njema kwa wahudumu wa umma wa kitambo walostaafu na wale waliotenda kazi yao kwa maadili mema na kwa moyo mweupe.<br>2.Kila afisi ya huduma za watu, PSC, na idara ya huduma z umma yafaa kuhakikisha kuwa kuna mpangilio mwafaka ya kutoka yanaoagazia kazi na kuelezewa kibinafsi na huduma za kuwekwa mahali.<br>3.Malipo ya uzeeni yanafaa kulipwa bila kuchelewa |
| 35 | Kufuatilia na kutoa ripoti kwa umma kuhusu hali ya maadili ya maisha kote nchini huku yakitolewa mafundisho ya maadili na uongozi wa umma. | 1. Tume ya Maadili na kupigana na ufisadi ilenge kusimamisha ugaidi wa kiuchumi na ipewe ulinzi kikatiba kama tume ya sura ya kumi na tano, hali kadhalika sehemu ya maadili ipokezwe tume ya maadili iliyopendekezwa na BBI. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 2. Tume hii iliyopewa mamlaka haya imshauri rais kuhusu viwango vya maadili kote katika maisha nchini.<br>3. Tume hii inafaa kufuatilia na kutoa ripoti kwa umma kuhusu viwango vya maadili kwa wafanyikazi wote wa umma.<br>4. Kuendeleza uchunguzi kimaadili, nidhamu na ubora wa kila sehemu ya serikali kila mwaka, na maoni ya wakenya na kasha kuweka wazi kwa umma matokeo yake. |
| 36 | Kuweka juhudi kali za kidijitali na kupigana na ufisadi kwenye sekta ya uuzaji na ununuzi wa ardhi ili kusaidia kutabiria wakenya ambao hufaidika kutokana ardhi. | 1. Kupiga ufisadi marufuku kwa hali ya juu katika manunuzi ya ardhi, kwenye bodi za ardhi, usajili wa ardhi, kwenye kanju na kwingineko.<br>2. Kuomba rais aelekeze hatua za kupigana na ufisadi kwenye sekta ya ununuzi na uuzaji wa ardhi na kutekeleza sharia hiyo kwa mpigo. |
| 37 | Kupunguza ushawishi unaoleta mgogoro katika huduma za umma na kwenye mashirika yasiyo ya kiserikali yasiyolipa kodi. | Kumalizia na kufanya sharia dhidi ya ushawishi uletao migogoro kenye huduma za umma na mashirika yasiyo ya kiserikali yasiyolipa kodi. |
| 38 | Wakenya waliliambia jopokazi kuwa ‘sekta ya mashirika yasiyo ya kiserikali hujidai kutoa nafasi za ajira. Na kwa kuwa tunang’ang’ana na ajira, tunang’ang’ana pia kukosoa shirika linalofanya makosa. Kunayo yaliyo mazuri na mengine ni mabaya.’<br>‘taabu za wakenya zinatumika kuwanyanyasa kwa faida ya mashirika yenyewe. Taabu hizi haziishi kwa kuwa kuna viinua mgongo vya kuzinyamazisha’ | 1. Misaada kutoka kwa mashirika haya nay a wafadhili iweze kufanyiwa ushiriki umma kama miradi mingineyo na pia izingatie sharia na sera zilizopo katika kutekeleza mipango yao.<br>2. Kusajili miradi yote ya mashirika haya na ya wafadhili kote nchini kwenye rejesta inayoweza kupatikana kwenye mitandao. Inafaa kuonyesha habari kuhusu mradi huo, malengo yake, maeneo ya kazi, kiwango cha fedha zilizotumika, wafadhili, na nambari ya uwasilianaji. |
| 39 | Kulinda, kuwezesha na kuheshimu wafuchuaji wa habari muhimu. | Wapewe tuzo na msaada wa kitaifa. |

**USALAMA NA ULINZI**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Sawazisha dhamani ya maisha ya wakenya kila sehemu ya nchi | Ni sharti tuache mazoea ya dhana kwamba kuna matokeo tofauti ya vurugu katika sehemu tofauti ya nchi. Kufanya mabadiliko haya kunahitaji usawa katika usambazaji wa maafisa wa polisi, mashtaka na juhudi za kuzuia uhalifu. |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Mkakatu wa usalama wa kitaifa unaojivuniwa na raia, inayomilikiwa na watu na inayoweza kabiliana na changamoto za tishio kwa wakenya | • Tunahitaji mbinu inayozingatia usalama wa kibinadamu iwekwe katika mkakati kamili wa kitaifa wa usalama wa ulinzi (kila baada ya maika miwili na kila rais anayeingia mamalakani katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kuchukua hatamun za uongozi) na ambayo inamilikiwa na watu na serikali yote. Inapaswa kuwa amilifu yenye kuzuia nay a kutahadharisha.<br>• Kuzuia na kujibu matishio ya dhana,kulinda mipaka ya Kenya<br>• Kupasha habari kwa usalama na kupigana na propaganda za adui.<br>• Kusitisha uwindaji wanyama pori na makabiliano ya kijamiii.<br>• Maadili, ufichuzi, na kupigana na ufisadi katika usalama.<br>• Kuzuia na kupigana na vurugu za kijinsia na familia.<br>• Upiganaji dhidi ya ugaidi, na kuzuia ugaidi na uhalifu wa kidunia na uhalifu wa kuunda pesa.<br>• Kupiga mkuki nafasi za kutoa usalama na kuhakikisha polisi wa Kenya wako kwa mgawo wa wananchi au wanazidi kiwango cha mgawo huo.<br>• Tahadhari za mapema za ugomvi na jinsi ya kukabiliana nazo na vita mipakani.<br>• Kulinda mazingira na sheria dhidi ya uwindaji wa wanyama pori.<br>• Usalama wa kitaifa wa mitandaoni. |
| 3 | Unganisha juhudi za kukabiliana na ugaidi kwa ulinzi wa ki- siasa, jamii,na utamaduni inayopunguza wanaoteuliwa, kupiga kisheriia matakwa ya adui, kuwazuia kudhibiti akili na fikra za wenye nchi. | 1. Imarisha uzuilifu wa ugaiodi kama ilivyowekwa katika mikakati ya kitaifa ya kupigana na ugaidi ili kuuzuia kwa kuzilaainisha idara husika, wizara na maajenti.<br>2. Patiana usiadizi wa usimamizi,kuendeleza na vitu kwa mipangilio ya kutenda ya kaunti ili kuzuia na kukabiliana na ugaidi wenye vurugu. |
| 5 | Angalia kukabiliana na ugaidi kama majibu ya kudumu na kuijenga katika dhana hiyo | Andaa Kenya dhidi ya magaidi kwa kutekeleza viwango vya kuzuia katika sekta zote, na sana sana majumba yanayotembelewa sana na raia ambayo ni ya kibinafsi. |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Gawa ulinzi kutoka kujibu hadi dharura za kitaifa na majanga. | 1. Unda nafasi za katibu wakuu tofauti kwa usalama wa kitaifa na dharura za kitaifa na majanga.<br>2. Kwa kupewa nafasi ya waziri mkuu katika mchakato huu, nafsi ya kikatiba ya katibu wa jopo la kiusalama wa kitaifa yafaa itumike kama mwenyekiti wa usalama wa kitaifa na kamati ya mawosia dhidi ya usalama. |
| 7 | Imarisha usimamizi wa bunge ya kitaifa ya usalama huku ukilinda habari na mienendo ya ulinzi wa kitaifa | Hakikisha wanakamati wa bunge kuhusu usalama wan chi, ulinzi na maswala ya kigeni wamechujwa vilivyo, kutathminiwa na jopo la ujasusi la kitaifa na kuapishwa chini ya kiapo cha siri. |
| 8 | Imarisha uongozi wa kitaifa wa usalama | Teua watu walio na historia njema ya utendakazi, na uzoefu wa kiusalama na ulinzi wa kitaifa, na uongozi bora. |
| 9. | Kutadhimini mahusiano ya kidiplomasia na mataifa yanayofadhili ugaidi, misimamo mikali ya kidini, na upanuzi au kujitenga. Hakikisha diplomasia imeundwa na kufadhiliwa ili kukabiliana na vitisho vinavyoibuka kabla ya kudai mwitiko madhubuti wa usalama. | Kuhusiana na bajeti, ni muhimu kwamba wizara ya masuala ya nje inapata mgao sawa na idara ya ulinzi, huduma ya kitaifa ya ujasusi na vyombo vingine vya kiusalama. |
| 10. | Kukabiliana na visa vya unyanyasaji wa kijinsia na ngono | Kupewe kipaumbele kwa kuzingatia na kutoa rasilimali maalum kwa polisi na kuchukua hatua za kuzuia dhuluma za kijinsia na ngono. |
| 11. | Hakikisha wakenya hawahatarishwi kwa majanga na hatari za mazingira na za kibinadamu | 1. Kwa kutekeleza mkakati kamili wa dharura za kitaifa, mkakati wa kushughulikia maafa na migogoro uliowekwa kwenye sheria ambayo inahusishwa na mipango ya kukiabiliana na majanga katika ngazi ya kaunti, kaunti ndogo na wadi ambayo husasishwa mara kwa mara. |
| 12 | Unda jopo ya kukabiliana na mizozo ya mipaka | 1. Shughulikia mizozo ya mipaka amabayo inahatarisha usalama wa kitaifa na jamii. Unda tume maalum au majopokazi kwa kila mzozo wa mpaka ili washauriane na wadau wote na kutoa mapendekezo ya mageuzi ambayo yatashughulikiwa. Kama mizozo ya mipaka baina ya meru-isiolo, meru-tharaka nithi, Baringo-turkana, Garissa-Tana river, Kisumu-Nandi, Laikipia-samburu, Turkana-West pokot, Kitui –meru, Makueni-machakos-Kajiado |

| | | |
|---|---|---|
| | | 2. Zuia migogoro ya kirasilimali kwa kuhakikisja mipaka ya kaunti imechorwa ili kuzidisha kugawa maji, malisho na raslimali zingine. |
| 13. | Imarisha imani na usalama wa wananchi wanaoripoti uhalifu na visa vinavyochangia kuzorota kwa usalama. | Ufichuzi na kuripoti yafaa kuwa na kinga dhabiti ili kuwalinda kujulikana, usiri na ulinzi wao  kuhusu kuripoti wanachi au mashahidi |
| 13 | Wafichuzi wa uhalifu walindwe | Wezesha taratibu za mahakama ambazo zitahahakikisha usalama na ulinzi wa watoaji habari, wafichuzi na mashahidi, hususan wa ugaidi, uhalifu mkubwa wa kimataifa, na ufisadi. |
| 14 | Imarisha uwezo wa kitaifa wa kukabiliana na usalama wa mitandaoni | Kulainisha katika ngazio za juu,ikiwemo jopo lka usalama wa kitaifa na kamati la wosia la kiusalama wa kitaifa, kuchukua majukumu ya kutilia nguvu ujuzi wa kukabiliana na usalama wa mitandaoni, sheria na taasisi. |
| 15 | Funga mianya chini ya anga iliyolindwa mbele ya uso na ukabiliani wa usalama kila sehemu ya Kenya. | Chora upya ramani kuhusu polisi na rasilimali kulingana na idadi ya watu na mahitaji ya ulinzi na kuanzisha mikakati ya kuwazuia polisi kutokana na kuhujumiwa na wahalifu waliojipanga vikundi. |
| 16. | Tilia ujuzi na kuzichunguza na kudhibiti kampuni za kibinafsi za usalama ili kutoa huduma nzuri na zenye kuambatana na usalama wa vitengo vya kitaifa. | 1. Jopo lenye mamlaka la kudhibiti kampuni za usalama za kibinafsi zipewe majukumu la kusimamia kampuni hizo.<br>2. Jopo hilo pia itoe maagizo maalum yanayoongozwa na viwango vya usalama vya taifa kwa kampuni hizo ili itekelezwe kikamilifu.<br>3. Kampuni za kibinafsi zafaa kushurutishwa kuwa na 50% ya wasimamizi iwe ni ya maafisa wa kiusalama waliostaafu au kujiuzulu kwa wema na maadili kutoka idara ya kitaifa ya usalama na vikosi vya nje, ili huduma zao ziwe sawa na zenye mwelekeo ufaao.<br>4. Tumia teknolojia kuunganisha ujumbe na habari kutoka kampuni za kibinafsi kwenda kwa makao makuu ya polisi wa taifa.<br>5. Unganisha CCTV za hoteli, majumba ya soko, na majumba yanayotembelewa sana na raia kwa CCTV za polisi wa kitaifa ili kuwezesha utekelezaji wa kazi mwema. |
| 17 | Linda wakenya wanaokaa karibu na mipaka ya nchi kutoka nchi jirani, wezi | Kwa usawa chora mipaka ya Kenya yote,zuia walinzi wa kigeni kutokana na kuingia humu |

| | | |
|---|---|---|
| | na waizi wa mifugo wanaotumia vurugu kuwagandamiza na kuwaibia wakenya wetu | nchini Kenya, Peana miundo misingi inayotosha, na kuimarisha vikosi katika mipakani mwa Kenya na kusimamia usalama wa wakenya wanaoishi mahali huko. |
| 18. | Utendakazi wa polisi ,na afya ya akili na ustawi. | 1.Fafanua viashiria, muhimu vya utenda kazi wa makamanda wa polisi kutoka ngazi ya inspekta jenerali wa polisi hadi chini kwa kitengo cha umma kuripoti takwimu za uhalifu wa kitaifa na ukosefu wa usalama. Vitengo hivi viwili vizingatiwe katika kupandisha vyeo na kutoa vivutio.<br>2. Piga marufuku ufisadi kastika kuwateua polisi kwa kuweka adhabu kali kwa wale wanaoingiza ufisadi katika zoezi la kuwateua makurutu.<br>3. Unga mkono maadili na utendakazi bora katika NPS kwa kutambua na kutuza ufanisi, kujituma na kujitolea kwa maafisa na wananchi.<br>4. Kama suala la kipaumbele, pawe na huduma za ushauri kuhusu afya na matibabu ya akili ya maafisa wa polisi. Polisi walio na majukumu makubwa amabyo yanawaweka katika hatari ya kudhurika kiakili wapewe mazingatio maalum. Hatua zote zinapaswa pia kuchukuliwa ili kuweka familia pamoja. |
| 19. | Utatuzi wa migogoro inayokumba wananchi. | Imarisha ujuzi wa raia raia wa kutatua migogoro na upatanishio katika mfumo mzima wa elimu ya Kenya. Fanikisha hili kwa kujumuisha maarifa ya utatuzi wa migogoro, mazungumzo na ushauri katika mtaala wa elimu katika ngazi zote za elimu ya msingi na sekondari. |
| 20. | Linda wakenya dhidi ya vyakula hatari na madawa au bidhaa zinazodhuru afya yao na maisha ya kimwili | Ongezea usalama wa chakula kwa ulinzi wa chakula.<br>1. Imarisha usimamizi wa usalama wa chakula kupitia kujumuisha na kuamanisha majukumu yaliyojirudia katika udhibiti wa uslama wa chakula na dawa.<br>2. Hakikisha wahudumu wa afya ya umma wamefanya kazi nyao inavyotakiwa.<br>3. Amanisha vidhibiti usalama wa chakula kwa wingi, inayozozana, na kujiangushania ili idhibitiwe kutoka mswada wa mbunge kuhusu jopo lenye mamlaka la kusimamia usalama wa chakula. |

| | | |
|---|---|---|
| 21 | Imarisha ghala la kitaifa la mahindi na kuitengezea wadhifa wa kuhifadhi chakula cha mifugo | Imarisha ghala la kitaifa, ifanye kuwa wazi, na iongezee iwe na uhifadhi wa chakula cha mifugo na wanyama wa nyumbani. |

\

**TUME NA MASUALA YANAYOGUSA KILA KIPENGEE.**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Kaunti ya Nairobi - Nairobi, ni kaunti tofauti na nyingine kutokana na ukweli kwamba ndio mji mkuu wa taifa ulio na afisi za umoja wa mataifa (UN). Afisi za UN jijini Nairobi ni makao makuu ya tatu ya umoja huo ulimwenguni. Ndio sababu ni tofauti na kaunti nyingine. Wakenya wanaustahi mji huu mkuu kuwa wenye vitengo vyote vikuu vya kiserikali na kama eneo muhimu kwa ushiriki wao wa mijadala ya uraia katika maisha ya kitaifa. Hii ina maana kuwa tume ya ugavi wa mapato inaweza kujitahidi kuzingatia hadhi hii maalum ya Nairobi na mahitaji ya huduma amabayo huja nayo. | Jopokazi linapendekeza kwamba Nairobi ipewe hadhi maalum ya mji mkuu ambao unaipa serikali ya kitaifa njia ya kutoa huduma na uwezeshaji ufaao katika kudumisha kama mji mkuu na kama kitovu cha kidiplomasia.<br><br>Wakati huo huo, hadhi maalum kama hiyo haifai kuzuia haki za wakazi wa Nairobi za uwakilishwaji katika ngazi za wadi na bunge. |
| 2. | Majukumu ya Seneti na bunge la kitaifa yafaa kutilia maanani mapendekezo ya kubadilisha uongozi wa nchi ilivyopendekezwa na jopo hili | Angalia tena kwa undani mipaka na uwiano wa uundaji sharia ili kuhakikisha majukumu ya mbunge kuu la kitaifa na seneti zimelingana na zile za muundo wa uongozi wan chi na mapendekezo mengine humu. |
| 3. | Tume ya maadili na kukabiliana na ufisadi | Gawanya jukumu la kiujasusi kutoka jukumu la kushurutisha maadili katika huduma za umma. Kazi ya kuripoti, kueneza na kutekeleza maadili itaendea tume iliyopendekezwa ya maadili katika sura ya maadili ya kitaifa. |
| 4 | Tume zafaa kuwajibika kwa wakenya | Ni sharti kila tume huru iwe na mifumo ya ndani ya uwajibikaji ambayo hutenganisha kwa njia huru na wazi mamlaka ya uteuzi na kupandisha vyeo na yale ya kusimamisha kazi na kusuta.<br><br>Juu ya hiyo, ukaguzi mkali wa mahesabu unaochunguza thamani ya matumizi ya pesa na kuendeleza kanuni bora za usimamizi wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | fedha za umma unapaswa kutumika kwa kila kitengo cha serikali na kila taasisi ya umma. |
| 5 | Imarisha kitengo cha uchunguzi wa uhalifu, ili kuwiana na uhuru wa uhalifu-mahakama idara inayohusisha kiongozi wa mashtaka ya umma na idara ya mahakama | Imarisha uwezo wa kiongozi wa uchunguzi wa uhalifu ili kufanya kazi yake pamoja na kiongozi wa mshataka ya umma. |
| 6 | Amanisha tume za usimamizi | Ili kurejesha vita vya mamlaka baina ya sura 15 ya tume, mfanye mweneyekiti kuwa yeye ndiye afisa mkuu mtendaji. Hili pendekezo yafaa kuhimizwa. |
| 7 | Kuwezesha kirasilimali sura ya 15 | 1. Tekeleza kiusimamizi ilivyopitishwa kikatiba kuhusu nusu ya makamishna katika sura ya 15 kuhusu tume, isipokuwa IEBC wanapaswa kuhudumu kwa muda maalum.<br>2. Kifungu cha 249(3) kimekiukwa na hili limeathiri uwezo wa tume za sura 15 na afisi huru kutekeleza ipasavyo na kwa njia nhuru majukumu yao. Wakati huo huo, tume na afisi huru pia zinapaswa kupitia ukaguzi mkali na mashirika yafaayo ili kuhakikisha kuwa zinatimiza majukumu yao kama inavyotakiwa. |
| 8 | Fanya uteuzi na uchunguzi kutathmini kwa sura ya 15 kuhusu tume ili kuhakikisha imehitimu matwakwa yanayotakikana na pia ripoti za maajenti wa serikali husika | Badilisha njia-fuata inayoleta uteuzi na uchunguzi ili iwe na habari kutoka idara ya serikali na ilazimu matakwa yote yawe yamefutwa. |
| 9 | Kuteua makamishna wa IEBC | Mkutano wa viongozi wa vyama vya kisiasa bungeni utateua kwa makubaliano, watu watakaopendekezwa kuteuliwa na Rais kama makamishna wa IEBC. Wanaosaka nafasi hizi wanapaswa kufikia vigezo vilivyoainishwa katika katiba na sheria na hawapaswi kuegemea upende wowote, na rekodi ya uadilifu na orodha waliyoiafiki, na ambao sio wanachama maarufu wa chama cha kisisasa na hawana rekodi ya kuchukua nafasi za umma kwa msaada wa chama. |
| 10. | Chakula cha Kenya chafaa kufikia kiwango chenye usalama | Unda taasisi madubuti iliyoungana ya kudhibiti na kuhakikisha usalama wa chakula. |
| 11 | Rahisisha na uweke udhibiti wazi | Bainisha majukumu ya mashirika ya udhibiti ili kuhakikisha kwamba hakuna urudiaji, na kurahisisha uwazi, pawe na huduma za haraka zinazopatikana gharama nafuu ili sheria ya udhibiti ifuatwe kwa kiwango vya juu. |

| | | |
|---|---|---|
| 12 | Kuimarisha majaribio ya serikali dhidi ya bidhaa zenye ubaya | Kuimarisha maabara ya kiserikali ili kuifanya iwe imara katika utekelezaji wa majukumu yake. |
| 13 | Jumuisha mabaraza ya usimamizi. Hivi sasa, karibu kila sheria huanzisha mamlaka fulani ya udhibiti au nyingine pia hubuni baraza fulani la rufaa kusuluhisha mambo yanayotokana na zoezi la wadhibiti wa mamalaka yake ya kisheria. Uhusiano kati ya mdhibiti na mabaraza haya umekosesha maana mantiki ya hukumu zisizioegemea upande wowote katika kuamua mzozo. Isitoshe, idadi kubwa ya mabaraza ya hukumu yaliyobuniwa kwa njia huishia kuvuja rasilimali za kitaifa pakubwa. | Inapendekezwa kuunda baraza moja ya rufaa ya kitaifa ambao itasikiza na kuamua kesi tofauti za rufaa (Kama vile, nguvu za umeme na kawi, michezo, na mazingira) |